BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MASWALI YA MTIHANI WA KUMALIZA ELIMU YA MSINGI MWAKA 2018

# MAARIFA YA JAMII

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MASWALI YA MTIHANI WA KUMALIZA ELIMU YA MSINGI 2018

# MAARIFA YA JAMII

*Kimechapwa na:*
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S. L. P. 2624,
Dar es Salaam, Tanzania.

© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2019

Haki zote zimehifadhiwa.

## YALIYOMO

DIBAJI ........................................................................................... iv
1.0 UTANGULIZI ........................................................................... 1
2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA KILA SWALI ........................................................................... 3
2.1. SEHEMU A........................................................................... 3
2.1.1. Kipengele I: Uraia ........................................................................... 3
2.1.2. Kipengele II: Historia........................................................................... 20
2.1.3. Kipengele III: Jiografia ........................................................................... 39
2.2. Sehemu B........................................................................... 54
3.0 UCHAMBUZI WA KUFAULU KWA WATAHINIWA KATIKA KILA MADA ........................................................................... 63
4.0 HITIMISHO........................................................................... 65
5.0 MAPENDEKEZO ........................................................................... 66
KIAMBATISHO ........................................................................... 68

## DIBAJI

Baraza la Mitihani la Tanzania linayo furaha kutoa taarifa ya uchambuzi wa majibu ya maswali ya Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi mwaka 2018 kwa somo la Maarifa ya Jamii. Taarifa hii imeandaliwa kwa lengo la kutoa mrejesho kwa watahiniwa, walimu, watunga sera, watunga mitaala na wadau wengine wa elimu. Majibu ya watahiniwa katika mtihani ni kiashiria kimojawapo kinachoonesha maarifa, stadi na mielekeo ambayo watahiniwa waliweza kupata au kutopata katika kipindi cha miaka saba ya Elimu ya Msingi.

Katika taarifa hii, mambo mbalimbali ambayo yamechangia watahiniwa kuweza au kushindwa kujibu maswali kwa usahihi yameainishwa. Uchambuzi unaonesha kuwa watahiniwa waliopata alama za juu za ufaulu walikuwa na maarifa ya kutosha na pia waliweza kubaini matakwa ya maswali ilhali watahiniwa waliopata alama za chini hawakuwa na sifa hizo hivyo walishindwa kujibu maswali kwa usahihi. Uchambuzi wa kila swali umefanyika na changamoto mbalimbali zilizowakabili watahiniwa wakati wa kujibu maswali zimeainishwa. Aidha, ulinganifu wa kiwango cha kufaulu kati ya mwaka 2017 na 2018 kwa kila mada umefanyika ili kuonesha kupanda au kushuka kwa kiwango cha kufaulu katika kila mada.

Baraza la Mitihani Tanzania lina imani kuwa mrejesho huu utawawezesha wadau mbalimbali wa elimu kuchukua hatua madhubuti ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji. Ni matumaini ya Baraza la Mitihani kuwa mamlaka husika zitahakikisha kuwa changamoto zilizoainishwa katika taarifa hii zinapatiwa ufumbuzi ili kuongeza ujuzi na maarifa kwa watahiniwa wanaotarajiwa kuhitimu elimu ya msingi mwaka huu na miaka ijayo.

Mwisho, Baraza la Mitihani linapenda kutoa shukrani za dhati kwa Maafisa Mitihani, na wengine wote waliohusika katika kuandaa taarifa hii.

**Dkt. Charles E. Msonde**
**KATIBU MTENDAJI**

## 1.0 UTANGULIZI

Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi (PSLE 2018) ulifanyika kati ya tarehe 05 na tarehe 06 ya mwezi Septemba, 2018. Katika mtihani huo, somo la Maarifa ya Jamii lilifanyika tarehe 06/09/2018. Jumla ya watahiniwa **957,904** walisajiliwa kufanya mtihani huu ambapo watahiniwa **944,159** sawa na asilimia **98.6** walifanya mtihani huo katika somo la Maarifa ya Jamii. Uchambuzi wa majibu ya mtihani wa Maarifa ya Jamii unaonesha kuwa watahiniwa **694,472** sawa na asilimia **73.62%** walifaulu mtihani huo katika somo hilo. Hata hivyo, uchambuzi huu haujawahusisha watahiniwa **6,164** ambao walifanya mtihani wa marudio.

Somo la Maarifa ya Jamii katika mtihani wa PSLE, 2018 lilikuwa na jumla ya maswali 40 ya kuchagua na 5 ya majibu mafupi yaliyokuwa yamegawanyika katika sehemu kuu mbili A na B. Sehemu A ilikuwa na maswali 40 ya kuchagua ambayo yalikuwa yamegawanyika katika vipengele vitatu. Kipengele cha I: Uraia – kilichokuwa na maswali 12, kipengele cha II: Historia – kilichokuwa na maswali 14 na kipengele cha III: Jiografia kilichokuwa na maswali 14. Sehemu B ilikuwa na maswali 5 ya majibu mafupi ambayo ni swali 1 la Uraia, maswali 2 ya Historia na maswali ya mwisho 2 ya somo la Jiografia.

Watahiniwa walitakiwa kujibu maswali yote kutoka katika sehemu zote mbili. Aidha, katika swali la 1 - 40 watahiniwa walipewa machaguo matano katika kila swali, ambayo kati yake kulikuwa na jibu sahihi. Watahiniwa walitakiwa kuchagua jibu sahihi na kisha kuweka kivuli katika herufi ya jibu sahihi katika fomu maalum ya kujibia (OMR). Katika kujibu swali la 41 – 45 watahiniwa walielekezwa kuandika majibu yao katika nafasi zilizoachwa wazi kwa kutumia kalamu ya wino wa bluu au mweusi.

Katika taarifa hii, herufi ya jibu sahihi imewekewa alama ya nyota (*) katika majedwali na chati. Zaidi ya hayo, asilimia ya watahiniwa ambao hawakufuata maelekezo ya namna ya kujibu swali iliwekwa katika uchambuzi na kupewa jina “Mengine” ikimaanisha watahiniwa ambao hawakujibu kabisa swali husika au walichagua jibu zaidi ya moja kama inavyoonekana katika majedwali na chati. Katika

uchambuzi huu, idadi ya watahiniwa na asilimia yao katika kila chaguo umeoneshwa. Ubora wa kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika kila swali utategemea idadi ya watahiniwa waliochagua jibu sahihi. Katika uchambuzi huu pia, sababu za watahiniwa kuchagua jibu, vipotoshi, kutojibu baadhi ya maswali au kuchagua jibu zaidi ya moja zimebainishwa.

Katika uchambuzi huu, ukokotoaji wa kiwango cha ufaulu utategemea idadi ya watahiniwa waliochagua au kuandika jibu sahihi kama ifuatavyo; endapo watahiniwa asilimia 0 hadi 39 ndio watakaokuwa wamechagua au kuandika jibu sahihi, ufaulu katika swali au mada hiyo utaelezwa kuwa ni hafifu. Kwa upande mwingine, endapo watahiniwa kati ya asilimia 40 hadi 59 watakuwa wamechagua au kuandika jibu sahihi, ufaulu katika swali hilo utaelezwa kuwa ni wa wastani. Aidha, ufaulu katika swali au mada utaelezwa kuwa mzuri endapo watahiniwa asilimia 60 au zaidi watakuwa wamechagua au kuandika jibu sahihi.

## 2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA KILA SWALI


### 2.1. SEHEMU A

#### 2.1.1 Kipengele I: Uraia

**Swali la 1:** Mtu anayedhibiti mwenendo wa wanafunzi shuleni ni

A Mwenyekiti wa Kamati ya Shule.
B Mwalimu wa nidhamu.
C Mwalimu mkuu msaidizi.
D Mwalimu wa taaluma.
E Mwalimu wa somo.

Swali hili lilitoka katika mada ya *Uongozi katika Ngazi ya Shule* na lililenga kupima uelewa wa watahiniwa juu ya majukumu ya mwalimu wa nidhamu shuleni. Kufaulu kwa watahiniwa kulikuwa kuzuri ambapo watahiniwa 641,455 (68.39%) waliweza kuchagua jibu sahihi B, *mwalimu wa nidhamu* kama Chati Na. 1 inavyoonesha.




**Chati Na. 1:** *Kufaulu kuzuri kwa watahiniwa katika swali la 1.*

Watahiniwa hawa walikuwa na ufahamu mzuri kuhusu uongozi katika ngazi ya shule hasa muundo wa uongozi na mgawanyo wa majukumu ya kiutendaji ya viongozi wa shule. Chaguo D, *mwalimu*

*wa taaluma* liliwavutia watahiniwa 115,199 (12.28%), ambao hawakufahamu kuwa mwalimu wa taaluma ndiye muhusika mkuu wa kusimamia shughuli zote za kitaaluma shuleni, hivyo basi watahiniwa walidhani kuwa mwalimu wa taaluma pia ana wajibu wa kudhibiti mwenendo wa wanafunzi shuleni.


Watahiniwa wengine walichagua vipotoshi vingine kama ifuatavyo: kipotoshi A, *Mwenyekiti wa kamati ya shule* (8.42%), watahiniwa hawakujua kuwa Mwenyekiti wa kamati ya shule jukumu lake kuu ni kuushauri uongozi wa shule kuhusu masuala mbalimbali ya maendeleo ya shule. Watahiniwa waliochagua kipotoshi C, *Mwalimu mkuu msaidizi* (7.41%) hawakufahamu kuwa majukumu ya Mwalimu mkuu msaidizi ni kuhifadhi kumbukumbu zote za mitihani kwa shule nzima na watahiniwa waliochagua kipotoshi E, *Mwalimu wa somo* (3.12%) hawakuwa na uelewa kuwa mwalimu wa somo amekabidhiwa jukumu la kufundisha somo husika. Kwa ujumla, watahiniwa hawa hawakuwa na uelewa wa namna muundo wa uongozi unavyokuwa na mgawanyo wa majukumu katika ngazi ya shule.

**Swali la 2:** Chombo cha juu katika maamuzi kwenye serikali ya kijiji ni

A Serikali ya kijiji.
B Kamati ya ulinzi na usalama.
C Mkutano Mkuu wa kijiji.
D Afisa Mtendaji wa kijiji.
E Kamati ya Maendeleo ya kijiji.

Swali lilitoka katika mada ya *Serikali za Mitaa* na watahiniwa walitakiwa kuchagua chombo cha juu kabisa katika kufanya maamuzi katika serikali ya kijiji. Kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kulikuwa hafifu ambapo watahiniwa waliobaini jibu sahihi walikuwa 189,722 (20.23%) kwa kuchagua jibu sahihi C, *Mkutano mkuu wa kijiji*. Mkutano Mkuu wa Kijiji ndicho chombo kikuu cha maamuzi katika ngazi ya kijiji na baadhi ya majukumu yake ni pamoja na kusimamia na kuwawajibisha watendaji katika ngazi ya kijiji, kujadili na kupokea au kukataa taarifa za utekelezaji wa shughuli za kijiji kutoka Halmashauri ya kijiji. Pia, Mkutano Mkuu wa kijiji una jukumu la kupokea, kujadili na kupitisha au kukataa taarifa

ya mapato na matumizi ya fedha za kijiji. Kwa ujumla, watahiniwa wote waliobaini jibu sahihi, walikuwa na uelewa mkubwa kuhusu muundo wa serikali ya kijiji na majukumu mbalimbali ya kamati za serikali ya kijiji. Chati Na. 2 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 2.




**Chati Na. 2:** *Kufaulu hafifu kwa watahiniwa katika swali la 2.*

Kwa upande mwingine, watahiniwa walishindwa kubaini chaguo sahihi kama ifuatavyo: watahiniwa 262,057 (27.94%) walichagua kipotoshi D, *Afisa Mtendaji wa Kijiji*, walishawishiwa na nafasi ya Afisa Mtendaji wa Kijiji (VEO) na wajibu wake wa kuandaa, kuitisha na kusimamia uendeshaji wa Mkutano Mkuu wa Kijiji akisaidiana na Mwenyekiti wa Kijiji. Watahiniwa 198,358 (21.15%) walichagua kipotoshi A, *Serikali ya kijiji*, watahiniwa hawa kwa mazoea yao walidhani kuwa Serikali ya kijiji ina mamlaka ya juu katika kufanya maamuzi kwa kuwa ndicho chombo cha utekelezaji wa shughuli za kila siku za wananchi kama kushiriki katika masuala ya ulinzi na usalama wa maisha na mali zao.

Watahiniwa (17.04%) waliochagua kipotoshi E, *Kamati ya Maendeleo ya kijiji*, walifikiri kuwa, kwa kuwa kamati hii inahusika na maendeleo ya kijiji, basi moja kwa moja itakuwa na mamlaka ya kutoa maamuzi katika ngazi ya kijiji. Pia, asilimia 12.96 ya watahiniwa waliochagua kipotoshi B, *Kamati ya ulinzi na usalama*

hawakujua majukumu na wajibu wa kamati hii ambayo ni kuhakikisha amani na usalama inakuwepo katika ngazi ya kijiji. Pia, walishindwa kuelewa kuwa taarifa za wananchi na mipango ya Serikali na taasisi zake hutolewa kupitia mikutano ya kijiji, na hawakujua kuwa mkutano mkuu wa kijiji una jukumu la kuthibitisha maamuzi yanayofanywa ama kuletwa na baraza la kijiji. Machaguo haya yamedhihirisha kuwa, watahiniwa hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu muundo wa serikali ya kijiji.

**Swali la 3**: Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya huchaguliwa na

A Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya.
B Baraza la Madiwani.
C Waziri katika Ofisi ya Rais.
D Afisa Mtendaji wa Kata.
E Wenyeviti wa Vijiji.

**Jedwali Na. 1: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

| Machaguo | A | B* | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 224,360 | 486,997 | 100,483 | 76,491 | 42,725 | 6,939 |
| Asilimia ya watahiniwa | 23.92 | 51.92 | 10.71 | 8.15 | 4.55 | 0.74 |

Swali hili ni kutoka katika mada ya *Serikali za Mitaa* na lilipima uelewa wa watahiniwa kuhusu namna ambavyo Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya anachaguliwa. Kama Jedwali Na. 1 linavyoonesha, kufaulu kwa watahiniwa kulikua kuzuri na watahiniwa wengi 486,997 (51.92%) waliweza kuchagua jibu sahihi B, *Baraza la Madiwani*. Watahiniwa walikuwa na uelewa kuwa Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya huchaguliwa na Baraza la madiwani la Wilaya husika.

Jumla ya watahiniwa 224,360 (23.92%) ambao walivutiwa na kipotoshi A, *Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya*. Hawakufahamu namna uchaguzi wa kidemokrasia unavyofanyika katika serikali za mitaa ambapo Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya huchaguliwa na Baraza la madiwani.


Kundi jingine la watahiniwa 100,483 (10.71%) walivutiwa na kipotoshi C, *Waziri katika Ofisi ya Rais*, hawakujua kwamba waziri hahusiki katika uteuzi wa Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya.

Vilevile, watahiniwa waliochagua vipotoshi D, *Afisa Mtendaji wa Kata* (8.15%) na E, *Wenyeviti wa Vijiji* (4.55%), hawakufahamu kuwa Afisa Mtendaji wa Kata ni mwajiriwa wa serikali na Wenyeviti wa Vijiji huchaguliwa na watu hivyo hawana madaraka ya moja kwa moja ya kumchagua Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya.

**Swali la 4:** Ipi kati ya sarafu zifuatazo ina picha ya Rais wa kwanza wa Zanzibar?

A Sarafu ya shilingi mia moja
B Sarafu ya shilingi mia mbili
C Sarafu ya shilingi hamsini
D Sarafu ya shilingi ishirini
E Sarafu ya shilingi kumi

Swali hili lilipima uwezo wa watahiniwa kutofautisha sarafu mbalimbali zinazotumika hapa nchini Tanzania. Swali lilitoka katika mada ya *Alama za Taifa* na kufaulu kwa watahiniwa kulikuwa kuzuri kama Chati Na.3 inavyoonesha.




**Chati Na.3:** *Kufaulu kuzuri kwa watahiniwa katika swali la 4.*


Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 937,995, kati yao watahiniwa 677,152 (72.19%) waliweza kuchagua jibu sahihi B, *sarafu ya shilingi mia mbili.* Jambo ambalo linaonesha kuwa watahiniwa walikuwa na uelewa wa alama mbalimbali zilizowekwa kwenye sarafu za Tanzania, Aidha, sarafu hii hutumiwa mara nyingi na watahiniwa kama nauli ya basi katika usafiri wa umma. Hivyo, baadhi ya wanafunzi huenda walitumia uzoefu wao wa kila siku katika maisha kubaini jibu sahihi.

Kwa upande mwingine, watahiniwa waliobaki walivutiwa na vipotoshi vingine walionesha kukosa maarifa kuhusu mada ya *Alama za Taifa* na sarafu za Tanzania hivyo kushindwa kubaini tofauti zake, kwa mfano, watahiniwa 104,917 (11.19%) waliochagua kipotoshi A, *sarafu ya shilingi mia moja,* hawakujua kuwa sarafu ya shilingi mia moja ina picha ya Baba wa taifa Marehemu J.K.Nyerere. Watahiniwa 66,680 (7.11%) walichagua C, *sarafu ya shilingi hamsini*, ambayo ina picha ya Rais mstaafu wa awamu ya pili A. H. Mwinyi; waliochagua E, *sarafu ya shilingi kumi* 44,051 (4.70%) ina picha ya Marehemu J.K. Nyerere na D, *sarafu ya shilingi ishirini* 40,195 (4.29%) ina picha ya Rais mstaafu A.H. Mwinyi.

**Swali la 5:** Maliasili zinazovutia watalii na kuchangia katika kukuza uchumi wa Taifa ni

A ardhi. B mito. C mifugo.
D madini. E mbuga za wanyama.

Swali hili lilitungwa kutoka katika mada ya *Uchumi Wetu* na lililenga kupima uelewa na uwezo wa watahiniwa kubainisha maliasili mbalimbali na michango yake katika kukuza uchumi wa Taifa. Kama Chati Na. 4 inavyoonesha swali hili lilijibiwa vizuri ambapo watahiniwa 771,981 (82.30%) walichagua jibu sahihi E, *mbuga za wanyama.*Tanzania imebahatika kuwa na mbuga za wanyama kama Serengeti, Ngorongoro na Selous ambazo zinavutia watalii kutoka sehemu mbalimbali duniani.




**Chati Na. 4:** *Kufaulu kwa kiwango kizuri (82.30%) kwa watahiniwa katika swali la 5.*

Watahiniwa hao waliweza kubaini jibu sahihi kwa kuwa walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu maliasili zinazovutai watalii na mada husika kwa ujumla wake na hii ilisaidia watahiniwa kutovutiwa na vipotoshi vilivyofanana kwa karibu.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 48,814 (5.20%) waliovutiwa na kipotoshi D, *madini*. Hawakuwa na ufahamu kuwa madini hayawavutii watalii, yanawavutia wawekezaji ingawa maliasili zote zinachangia ukuaji wa uchumi wa Taifa. Pia, watahiniwa walivutiwa na kipotoshi hiki kwa sababu ya taarifa za sekta hii kutawala vyombo vya habari hivi karibuni kuhusu serikali kusimamisha usafirishaji wa makinikia nje ya nchi.

Zaidi ya hayo, watahiniwa 45,650 (4.87%) walichagua kipotoshi A, *ardhi*. Ardhi ni kigezo kikubwa cha ukuzaji wa uchumi lakini mara nyingi huvutia wawekezaji na sio watalii. Watahiniwa waliobaki walichagua vipotoshi B, *mito* (3.11%) na C, *mifugo* (3.95%) hawakuwa na ufahamu kuhusu maliasili zinazovutia watalii nchini Tanzania.

**Swali la 6:** Wajibu wa serikali katika kujenga maadili ya viongozi ni

A kuwakopesha magari viongozi wote
B kuimarisha mfumo wa chama kimoja cha siasa
C kusimamia sheria za utumishi wa umma
D kuhamisha watumishi wasio waadilifu

E kuajiri watumishi wenye elimu ya juu tu.

**Jedwali Na. 2: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

| Machaguo | A | B | C* | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 32,757 | 168,161 | 580,098 | 89,467 | 61,646 | 5,866 |
| Asilimia ya watahiniwa | 3.49 | 17.93 | 61.84 | 9.54 | 6.57 | 0.63 |

Swali hili liliandaliwa kutoka katika mada ya *Demokrasia* mada ndogo ya *Utawala Bora*, swali lilipima ufahamu wa watahiniwa kuhusu wajibu wa serikali katika kukuza maadili ya viongozi. Jedwali Na. 2 linaonesha watahiniwa wengi walifaulu kwa kiwango kizuri kwani asilimia 61.84,ya watahiniwa waliweza kuchagua jibu sahihi ambalo ni C, *kusimamia sheria za utumishi wa umma*. Watahiniwa hawa walionesha uelewa kuwa serikali inao wajibu wa kukuza maadili ya viongozi na njia mojawapo ya kujenga maadili ya umma ni kusimamia sheria za utumishi wa umma.

Mbali na hao, watahiniwa 168,161 (17.93%) waliochagua kipotoshi B, *kuimarisha mfumo wa chama kimoja cha siasa*, hawakuwa na ufahamu kuwa badala ya kuimarisha mfumo wa chama kimoja, sheria za utumishi wa umma zinasaidia kurekebisha maadili ya viongozi na watumishi wa umma kwa ujumla.

Watahiniwa wengine walichagua vipotoshi vingine kama ifuatavyo: kipotoshi D, *kuhamisha watumishi wasio waadilifu* (9.54%); watahiniwa walishindwa kuelewa kuwa kuhamisha watumishi wasio waadilifu haisaidii kuondoa tatizo isipokuwa itakuwa ni kuhamisha tatizo kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine ambako linaweza kusambaa hadi kwa watumishi wengine wa umma. Watahiniwa waliochagua kipotoshi E, *kuajiri watumishi wenye elimu ya juu tu* (6.57%) walishindwa kuelewa kuwa maadili hayahusiani na kiwango cha elimu cha kiongozi, maadili ni tabia iliyojengeka ndani ya nafsi ya mtu binafsi. Kipotoshi A, *kuwakopesha magari viongozi wote* (3.49%), hawakufahamu kuwa maadili ya viongozi hayajengwi kwa kutoa mikopo bali kwa kuweka mifumo na taratibu zinazosimamia utendaji wa kila siku katika utumishi wa umma. Kwa ujumla, watahiniwa walioshindwa kubaini jibu sahihi walikuwa na

uelewa mdogo kuhusu majukumu ya serikali katika kuwajengea maadili viongozi.

**Swali la 7:** Tofauti kati ya mila na desturi ni

A mila hubadilika mara kwa mara kuliko desturi.
B desturi hubadilika mara kwa mara kuliko mila.
C mila ni mazoea wakati desturi ni vitendo.
D mila ni mazoea na huweza kubadilika na kuwa desturi.
E desturi hubadilika mara kwa mara kuliko mazoea.

**Jedwali Na. 3: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

| Machaguo | A | B* | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 159,003 | 266,592 | 312,179 | 150,692 | 40,990 | 8,539 |
| Asilimia ya watahiniwa | 16.95 | 28.42 | 33.28 | 16.07 | 4.37 | 0.91 |

Swali hili liliandaliwa kutoka katika mada ya *Utamaduni Wetu* na watahiniwa walitakiwa kuonesha tofauti kati ya mila na desturi. Kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili ni hafifu kama Jedwali Na 3 linavyoonesha, ambapo jumla ya watahiniwa 266,592 (28.42%) waliweza kubaini jibu sahihi B, *desturi hubadilika mara kwa mara kuliko mila*. Watahiniwa hawa walionesha ufahamu kuhusu vipengele vya utamaduni, hususani vielelezo mbalimbali vya utamaduni kwa kubaini kuwa desturi inahusisha tabia na mwenendo ambao huweza kubadilika kulingana na wakati na mila haziwezi kubadilika kwa urahisi kwa sababu hurithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 312,179 (33.28%) walichagua kipotoshi C, *mila ni mazoea wakati desturi ni vitendo*. Watahiniwa walishindwa kutofautisha kati ya mila na desturi. Mila ni mazoea yanayorithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine kama vile taratibu za kuoa, mazishi na sherehe za kimila. Desturi ni mambo ya mazoea yanayotendwa kila siku na jamii kama vile kumsalimia mtu anayekuzidi umri kwa kusema ‘*shikamoo*’, kupeana mikono na kubisha hodi mlangoni.


Watahiniwa waliochagua kipotoshi A, *mila hubadilika mara kwa mara kuliko desturi* walikuwa 159,003 (16.95%). Watahiniwa waliovutiwa na kipotoshi hiki walikuwa hawana maarifa juu ya tofauti kati ya mila na desturi hivyo kutumia maneno mawili kwa wakati mmoja kumaanisha kitu kilekile.

Aidha, kundi la watahiniwa 150,692 (16.07%) waliovutiwa na kipotoshi D, *mila ni mazoea na huweza kubadilika na kuwa desturi*, walikosa maarifa ya mada ya vipengele vya utamaduni. Zaidi, kuna watahiniwa 40,990 (4.37%) waliochagua kipotoshi E, *desturi hubadilika mara kwa mara kuliko mazoea*. Watahiniwa hao walishindwa kuelewa kuwa desturi na mazoea wakati mwingine hutumiwa kumaanisha kitu kilekile ambapo mazoea ni matukio au maarifa yatumiwayo na watu wa jamii fulani, ambayo yanamsaidia mtu kufikiri na kujiheshimu katika jamii, na desturi ni mambo yote yanayokubalika katika jamii.

**Swali la 8:** Matumizi ya ofisi ya umma kwa manufaa binafsi huitwa

A takrima. B rushwa. C uzalendo.
D ubinafsi. E ujasiriamali.

Lengo la swali hili ni kupima uelewa wa watahiniwa kuhusu maadili miongoni mwa watumishi wa umma hasa matumizi mabaya ya ofisi za umma kwa manufaa binafsi. Swali hili lilitoka katika mada ya *Demokrasia* hususani mada ndogo ya *Utawala Bora*. Kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kilikuwa hafifu kama ilivyooneshwa katika Chati Na. 5 ambapo watahiniwa 238,522 (25.43%) tu waliweza kubaini jibu sahihi B, *rushwa*.




**Chati Na. 5:** *Kufaulu kwa kiwango hafifu (25.43%) kwa watahiniwa waliofanya swali hili.*

Watahiniwa walioweza kubaini jibu sahihi walikuwa na ufahamu mzuri wa mada na mahitaji ya swali. Pamoja na maarifa yao ya darasani watahiniwa waliweza kuhamisha maarifa yao ya maisha ya kila siku na kuweza kubaini jibu sahihi kutokana na kampeni za serikali zinazoendelea za kupambana na rushwa katika utumishi wa umma.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 229,933 (24.51%) walichagua D, *ubinafsi*. Watahiniwa waliovutiwa na kipotoshi hiki hawakufahamu kuwa ubinafsi ni hali ya mtu kujifikiria na kujipenda mwenyewe na haina uhusiano na matumizi ya ofisi ya umma kwa manufaa binafsi.

Zaidi ya hayo, watahiniwa 178,256 (19.00%) walichagua A, *takrima*, watahiniwa waliochagua kipotoshi hiki hawakuelewa kuwa takrima ni ukarimu auoneshao mtu kwa rafiki au mtu mwingine na hutolewa bila kutarajia malipo. Pia, watahiniwa 154,143 (16.43%) waliochagua E, *ujasiriamali* hawakua na uelewa kuwa ujasiriamali ni kutafuta fursa na kuzitumia pasipo kuhofia hasara. Watahiniwa hawa hawakuwa na ufahamu wa dhana ya ujasiriamali hivyo kushindwa kutofautisha kati ya ujasiriamali na rushwa. Mbali na hao, watahiniwa 129,180 (13.77%) waliochagua C, *uzalendo* hawakufahamu kuwa uzalendo ni hali ya kuipenda nchi yako na

kuwa tayari kuilinda. Kwa ujumla, watahiniwa wote walioshindwa kubaini jibu sahihi hawakuwa na maarifa ya kutosha kujibu swali hili kwa usahihi.

**Swali la 9:** Zipi kati ya nchi zifuatazo ni wanachama wa Jumuiya ya Madola?

A Botswana na Burundi
B Msumbiji na Rwanda
C Kenya na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo
D Malawi na Burundi
E Zambia na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo

**Jedwali Na.4: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

| Machaguo | A | B* | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 201,706 | 224,646 | 251,456 | 133,114 | 115,027 | 12,046 |
| Asilimia ya watahiniwa | 21.50 | 23.95 | 26.81 | 14.19 | 12.26 | 1.28 |

Swali hili lilitungwa kutoka katika mada ya *Ushirikiano kati ya Tanzania na Mataifa Mengine* na lililenga kupima uelewa wa watahiniwa kuhusu Jumuiya ya Madola ambapo watahiniwa walitakiwa kubaini wanachama wa jumuiya hiyo. Jumuiya ya Madola ni muungano wa nchi mbalimbali (54) ambazo zilikuwa makoloni ya dola ya Uingereza na ilianzishwa tangu mwaka 1931. Kama ilivyooneshwa katika Jedwali Na 4, Kufaulu kwa watahiniwa kulikuwa hafifu ambapo jumla ya watahiniwa 224,646 (23.95%) waliweza kubaini jibu sahihi kwa kuchagua B, *Msumbiji na Rwanda*. Watahiniwa hawa walikuwa na maarifa kuhusu Jumuiya ya Madola na wanachama wake. Msumbiji ina historia ya kuvutia kwenye Jumuiya ya Madola, kwa sababu Msumbiji ilikuwa ni koloni la Wareno ila mwaka 1995 walipitishwa kuwa wanachama wa kwanza wa Jumuiya ya Madola kwa nchi zisizo na historia yoyote na Uingereza, na Rwanda walijiunga na umoja huu mwaka 2009 na kuwa nchi ya pili isiyo na uhusiano wa kihistoria na Uingereza. Kwa ujumla, watahiniwa waliochagua jibu sahihi walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu wanachama wa Jumuiya ya Madola hususani nchi wanachama ambazo hazikutawaliwa na Uingereza.


Kwa upande mwingine, watahiniwa 251,456 (26.81%) walichagua jibu lisilo sahihi C, *Kenya na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo*. Watahiniwa hawa hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu wanachama wa Jumuiya ya Madola kwa sababu Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo si mwanachama wa jumuiya hiyo kwa kuwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo haina uhusiano wa kihistoria na Uingereza.

Zaidi ya hayo, watahiniwa 201,706 (21.50%) walichagua kipotoshi A, *Botswana na Burundi*. Burundi si mwanachama wa jumuiya ya Madola ingawa imetangaza rasmi nia ya kuwa mwanachama wa jumuiya, yawezekana hii ndio sababu iliyowashawishi watahiniwa kukichagua kipotoshi hiki. Mbali na hayo, watahiniwa 133,144 (14.19%) walichagua kipotoshi D, *Malawi na Burundi,* na watahiniwa wengine 115,027 (12.26%) walichagua kipotoshi E, *Zambia na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo*, ambapo Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo sio mwanachama wa Jumuiya ya madola kwa sababu hawakutawaliwa na Uingereza bali walitawaliwa na Ufaransa na Ubelgiji. Watahiniwa wote waliochagua vipotoshi hivi hawakuwa na maarifa kuhusu Jumuiya ya Madola na wanachama wake.

**Swali la 10:** Moja ya matukio yanayokiuka Haki za Binadamu nchini Tanzania ni

A mauaji ya vikongwe na maalbino.
B ukataji na upandaji miti.
C kuwafungulia mashtaka wahalifu.
D kufukuzwa kazi viongozi wasio waadilifu.
E serikali kusimamia ukusanyaji wa kodi.

Swali lililenga kupima uelewa wa watahiniwa kuhusu utekelezaji wa Haki za Binadamu nchini Tanzania. Swali liliwataka watahiniwa kubaini tukio moja la uvunjifu wa haki za binadamu nchini Tanzania kati ya mengi yaliyoorodheshwa. Watahiniwa walio wengi walionesha uelewa wa matukio ya uvunjaji wa haki za binadamu nchini Tanzania kama ilivyooneshwa katika Chati Na 6.




**Chati Na. 6:** *Kufaulu kwa kiwango kizuri (81.72%) kwa watahiniwa katika swali la 10.*

Watahiniwa 766,505 (81.72%) waliweza kuchagua jibu sahihi A, *mauaji ya vikongwe na maalbino*. Watahiniwa walikuwa na ufahamu wa dhana ya haki za binadamu ambapo msingi mmojawapo wa haki za binadamu ni haki ya kuishi. Aidha, waliweza kubaini jibu sahihi, kwa sababu ya kuwepo kwa kampeni mbalimbali dhidi ya mauaji ya vikongwe na maalbino kupitia serikali na mihadhara mbalimbali kama vile vyombo vya habari, vyama vya siasa na mashirika yasiyo ya kiserikali. Hivyo, ilikuwa rahisi kwa watahiniwa kuhamisha maarifa ya nje ya darasa na kubaini jibu sahihi.


Kwa upande mwingine, jumla ya watahiniwa 46,397 (4.95%) ambao walivutiwa na kipotoshi D, *kufukuzwa kazi viongozi wasio waadilifu* walishindwa kuelewa mahitaji ya swali, hawakufahamu kuwa hatua za kinidhamu dhidi ya viongozi wasio waadilifu huchukuliwa kwa kufuata miongozo ya utumishi wa umma. Watahiniwa wengine 43,289 (4.62%) waliovutiwa na kipotoshi B, *ukataji na upandaji wa miti* pia hawakuwa na ufahamu wa dhana ya haki za binadamu kwani jibu hili halikuwa na uhusiano wowote na swali lililoulizwa. Zaidi ya hayo, watahiniwa 39,021 (4.16%) walivutiwa na kipotoshi E, *serikali kusimamia ulipaji wa kodi*. Watahiniwa hawa hawakufahamu kuwa kulipa kodi ni wajibu wa kila raia na serikali kusimamia ulipaji

wa kodi hakuna uhusiano na uvunjifu wa haki za binadamu nchini Tanzania. Watahiniwa wengine 36,961 (3.94%) walivutiwa na kipotoshi C, *kuwafungulia mashtaka wahalifu*, watahiniwa hawa hawakufahamu kuwa moja ya nguzo za utawala wa sheria ni kuwafikisha mbele ya vyombo vya sheria watuhumiwa wa uhalifu. Hivyo, hakuna uhusiano wa kipotoshi na uvunjifu wa haki za binadamu.

**Swali la 11:** Mojawapo ya njia ambazo wananchi wanaweza kushiriki katika ulinzi na usalama ni

A kupiga wahalifu.
B kufanya mazoezi ya viungo.
C kuwaua wahalifu.
D kuwafichua wahalifu.
E kuwa urafiki na wahalifu.

Swali hili lilitoka katika mada ya *Ulinzi na Usalama* na liliwataka watahiniwa kubaini mojawapo ya njia ambazo wananchi wanaweza kushiriki katika ulinzi na usalama. kama ilivyooneshwa kwenye Chati Na 7. Kufaulu kwa watahiniwa kulikuwa kuzuri ambapo, watahiniwa 622,224 (66.34%) walichagua jibu sahihi D, *kuwafichua wahalifu*. Watahiniwa hawa walikua na maarifa kuhusu ulinzi na usalama, hasa mbinu za kudumisha amani na usalama katika jamii. Kwa ujumla wajibu wa kikatiba wa raia mwema ni pamoja na kutoa taarifa kwa vyombo vya ulinzi na usalama jambo lolote linaloashiria uhalifu.




**Chati Na. 7:** *Kufaulu kuzuri kwa watahiniwa katika swali la 11.*

Kwa upande mwingine, Kipotoshi A, *kupiga wahalifu* kiliwavutia watahiniwa 125, 786 (13.41%) kwa sababu ya kuwepo kwa tabia ya baadhi ya watu wachache katika jamii kujichukulia sheria mkononi. Pia, jumla ya watahiniwa 89,391 (9.53%) ambao walivutiwa na kipotoshi B, *kufanya mazoezi ya viungo* walishindwa kuelewa mahitaji ya swali na walikosa maarifa kuhusu ulinzi na usalama.

Watahiniwa wengine 58,650 (6.25%) ambao walivutiwa na C, *kuwaua wahalifu* hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada na walishawishiwa na tabia ya jamii kujichukulia sheria mkononi kwa kuwaua wahalifu pasipo kuwapeleka mahakamani. Pia, watahiniwa 35,742 (3.81%) walivutiwa na E, *kuwa urafiki na wahalifu* na yawezekana watahiniwa hawa walichagua jibu hili kwa sababu ya kuwepo kwa baadhi ya familia katika jamii ambazo hushirikiana na watuhumiwa katika makazi yao.

**Swali la 12:** Viashiria vya utandawazi ni pamoja na

A kupungua kwa tofauti ya kipato.
B uchumi wa soko huria.
C kupungua kwa umaskini.
D kuwepo kwa ushindani wa kutengeneza silaha.
E kuwepo kwa bidhaa nyingi toka viwanda vya ndani.

**Jedwali Na. 5: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

| Machaguo | A | B* | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 86,308 | 463,893 | 117,445 | 84,163 | 177,520 | 8,666 |
| Asilimia ya watahiniwa | 9.20 | 49.46 | 12.52 | 8.97 | 18.93 | 0.92 |

Swali hili liliandaliwa kutoka katika mada ya *Utamaduni wa Tanzania na Tamaduni Nyingine* na swali liliwataka watahiniwa kubaini viashiria vya utandawazi. Kama ilivyooneshwa katika Jedwali Na 5, kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kulikuwa kwa wastani ambapo, watahiniwa 463,893 (49.46%) waliweza kubaini jibu sahihi B, *Uchumi wa soko huria*. Watahiniwa hawa walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu utandawazi kwani vipotoshi vilivyo vingi vilishabihiana na jibu sahihi kwa ukaribu mkubwa. Uchumi wa soko

huria huongozwa na nguvu za soko ambazo ni ugavi na utashi, katika utandawazi nafasi ya serikali katika kusimamia uchumi ni finyu hivyo basi, uzalishaji mali na utoaji wa huduma mbalimbali unategemea mahitaji ya soko yaliyopo kwa wakati husika.

Kipotoshi E, *kuwepo kwa bidhaa nyingi kutoka viwanda vya ndani* kiliwavutia watahiniwa 177,520 (18.93%). Watahiniwa waliochagua kipotoshi hiki hawakufahamu kuwa lengo kuu la utandawazi ni kuzifanya nchi zinazoendelea kuwa soko la bidhaa za viwanda kutoka nchi zilizoendelea. Watahiniwa 117,445 (12.52%) ambao walivutiwa na kipotoshi C, *kupungua kwa umaskini* hawakufahamu kuwa utandawazi haujatoa suluhisho la umaskini katika nchi zinazoendelea. Yawezekana baadhi ya watahiniwa waliovutiwa na kipotoshi hiki walihusisha utandawazi na misaada mbalimbali itolewayo na nchi wafadhili kama vile nchi ya Marekani na kuongezeka kwa mashirika mbalimbali yasiyo ya kiserikali na mashirika ya kimataifa yanayojihusisha na kupunguza umaskini nchini Tanzania kama Shirika la Maendeleo la Marekani (USAID).

Jumla ya watahiniwa 86,308 (9.20%) walivutiwa na kipotoshi A, *kupungua kwa tofauti ya kipato*. Watahiniwa waliochagua kipotoshi hiki hawakuwa na ufahamu wa madhara ya utandawazi katika nchi zinazoendelea ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa tofauti ya kipato kati ya walionacho na wasionacho ambapo utajiri hulimbikizwa mikononi mwa watu wachache. Ingawa, hii inategemeana sana na sera za serikali za namna ya kupunguza madhara ya utandawazi. Watahiniwa wengine 84,163 (8.97%) waliovutiwa na kipotoshi D, *kuwepo kwa ushindani wa kutengeneza silaha* hawakuwa na ufahamu kuwa ushindani wa kutengeneza silaha ulichochewa na kuwepo kwa vita baridi kati ya nchi za magharibi na nchi za mashariki. Baada ya kusambaratika kwa kambi ya nchi za mashariki katika miaka ya 1980 vita baridi imepungua kwa kiasi kikubwa hivyo hata ushindani wa kutengeneza silaha umepungua pia. Kwa misingi hiyo, hakuna uhusiano wa suala la ushindani wa kutengeneza silaha na viashiria vya utandawazi.

### 2.1.2 Kipengele II: Historia

**Swali la 13:** Baba wa baba yako anaitwa

A baba. B mjukuu. C mjomba.
D babu. E mpwa.

**Jedwali Na. 6: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

| Machaguo | A | B | C | D* | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya watahiniwa | 34,364 | 32,245 | 24,514 | 824,464 | 17,959 | 4,449 |
| Asilimia ya Watahiniwa | 3.66 | 3.44 | 2.61 | 87.90 | 1.91 | 0.47 |

Swali liliwataka watahiniwa kubaini jina la baba wa baba. Ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri kwani watahiniwa 824,464 (87.90%) waliweza kuchagua jibu sahihi D, *babu*. Babu hufanya majukumu makubwa kama vile kuendeleza umoja, kufundisha maarifa, tunu na hekima katika familia kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Pia, babu wana upendo na wanaaminiwa na wajukuu zao. Hivyo, maarifa ya kutosha kuhusu mti wa familia unaonesha asili ya ukoo, uhusiano wa kifamilia pamoja na uwezo wa kuhawilisha maarifa viliwawezesha watahiniwa hawa kubaini na kuchagua jibu sahihi.

Hata hivyo, jumla ya watahiniwa 109,082 (11.62%) walichagua vipotoshi: A, *baba*; B, *mjukuu*; C *mjomba* na E, *mpwa*. Uchaguzi wa vipotoshi hivyo unathibitisha kwamba watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha ya jamaa na mahusiano katika familia pana. Kwa ujumla, watahiniwa walipaswa kufahamu kwamba “baba” ni mzazi wa kiume; “mjukuu” ni mtoto wa mtoto wako; “mjomba” ni kaka wa mama au baba na “mpwa” ni mtoto wa kiume wa kaka au dada.

**Swali la 14:** Ni Taifa lipi la kibepari liliitawala Tanganyika kuanzia mwaka 1891 hadi 1918?

A Ujerumani B Uingereza C China
D Ureno E Ufaransa

**Jedwali Na. 7: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

| Machaguo | A* | B | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahinwa | 531,565 | 221,787 | 40,357 | 79,644 | 58,068 | 6,574 |
| Asilimia ya Watahiniwa | 56.67 | 23.64 | 4.30 | 8.49 | 6.19 | 0.70 |

Swali lilitungwa kutoka kutoka mada ya *Kuanzishwa kwa Utawala wa Kikoloni Tanganyika na Zanzibar*. Swali lilipima uwezo wa watahiniwa kutambua taifa la kibepari lililotawala Tanganyika toka mwaka 1891 hadi 1918. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa ni wa kiwango cha wastani kwani watahiniwa 531,565 (56.67%) waliweza kuchagua jibu sahihi A, *Ujerumani*. Watahiniwa hawa walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu kugombaniwa na kugawanywa kwa Bara la Afrika miongoni mwa mataifa ya kibepari mnamo karne ya 19. Aidha, watahiniwa hawa walikuwa na ufahamu wa kutosha kuhusu mataifa ya kikoloni yaliyotawala makoloni mbalimbali ya Afrika ikiwemo Tanganyika. Kwa hakika, watahiniwa hawa walikuwa na ufahamu wa vipindi ambavyo Tanganyika ilipitia tangu kugombaniwa na mataifa ya Ulaya hadi ilipojitawala yenyewe.

Aidha, watahiniwa 221,787 (23.64%) walichagua B, *Uingereza*. Uchaguzi wa kipotoshi hicho unaweza kuwa ulisababishwa na umaarufu wa Uingereza katika historia ya Tanganyika miongoni mwa watahiniwa. Hii inathibitishwa na ukweli kwamba Uingereza ni taifa la Ulaya ambalo liliitawala Tanganyika kwa zaidi ya miaka arobaini kuanzia 1919 hadi 1961 na ndio taifa lililokabidhi uhuru kwa Tanganyika mwaka 1961. Kwa ujumla, watahiniwa waliochagua kipotoshi hicho walitambua mataifa yaliyoitawala Tanganyika lakini walishindwa kutambua kipindi maalumu cha kila mtawala wa kikoloni.

Jumla ya watahiniwa 40,357 (4.30%) walichagua C, *China.* Watahiniwa hawa hawakuwa na maarifa ya kutosha katika kuanzishwa kwa utawala wa kikoloni Tanganyika na Zanzibar. Watahiniwa hawa walipaswa kufahamu kuwa China haikutawala Tanganyika ingawaje ilisaidia Tanzania katika ujenzi wa reli ya


TAZARA katika kipindi cha miaka ya 1970 na kwa sasa, China ni mshirika mkubwa wa Afrika kibiashara.

Machaguo mengine D, *Ureno* na *E, Ufaransa* yalichaguliwa na watahiniwa ambao hawakuwa na maarifa ya kutosha juu ya mada husika. Ni ukweli kwamba Ureno na Ufaransa zilihusika katika Afrika Mashariki kabla ya ukoloni, lakini hakuna taifa kati ya hayo lililoitawala Tanganyika katika kipindi hicho. Kwa ujumla, watahiniwa hao hawakuwa na ufahamu wa mataifa yaliyotawala Tanganyika. Kwa mfano, watahiniwa hao walipaswa kufahamu kuwa Ureno ilitawala pwani ya Afrika Mashariki kati ya karne 15 hadi 17 tofauti na swali ambalo lilijikita karne za 19 na 20. Hivyo, si sahihi kusema kwamba taifa la Ureno lilitawala Tanganyika kati ya mwaka 1891 hadi 1918.

**Swali la 15 :** Ni kwa nini Berlin ni miongoni mwa miji maarufu katika historia?

A ni Makao Makuu ya Umoja wa Mataifa
B ni Makao Makuu ya Jumuia ya Madola
C ni mji uliokuwa kitovu cha biashara ya utumwa
D ni mji wa Ufaransa ulioendesha utawala wa kulisha kasumba
E ni mji ambapo mgawanyo wa Bara la Afrika ulifanyika

Swali hili lilitungwa kutoka kwenye mada ya *Uvamizi wa Kikoloni Barani Afrika tangu miaka ya 1880* na liliwataka watahiniwa kubaini sababu inayoufanya mji wa Berlin kuwa miongoni mwa miji maarufu katika historia. Kwa ujumla, kiwango cha kufaulu katika swali hili kilikuwa ni kizuri kwani watahiniwa 613,212 (65.37%) waliweza kuchagua jibu sahihi E, *ni mji ambapo mgawanyo wa Bara la Afrika ulifanyika*. Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu kugombaniwa na kugawanywa kwa bara la Afrika miongoni mwa mataifa ya Ulaya. **Chati Na. 8** inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili.




**Chati Na. 8**: *Inaonesha kufaulu kwa kiwango kizuri (65.37 %) kwa watahiniwa waliofanya swali hili.*

Hata hivyo, jumla ya watahiniwa 319,951 (34.11%) waliochagua vipotoshi: A, ni *Makao Makuu ya Umoja wa Mataifa* ; B, *ni Makao Makuu ya Jumuia ya Madola*; C, *ni mji uliokuwa kitovu cha biashara ya utumwa* na D, *ni mji wa Ufaransa ambao uliendesha utawala wa kulisha kasumba* hawakuwa na maarifa ya kutosha juu ya uvamizi wa wakoloni Barani Afrika mnamo miaka ya 1880, ushirikiano wa kimataifa, biashara ya utumwa na mifumo ya utawala wa kikoloni. Watahiniwa hao walipaswa kufahamu kwamba makao makuu ya Umoja wa Mataifa yapo New York (Marekani), makao makuu ya Jumuiya Madola yapo London (Uingereza). Zaidi ya hapo, watahiniwa walipaswa kufahamu kwamba Berlin haikuwahi kuwa kitovu cha biashara ya utumwa au mji wa Ufaransa ambao uliendesha utawala wa kulisha kasumba.

**Swali la 16 :** Mataifa makubwa ya kibepari yaliyogombania Bara la Afrika yalikuwa

A Uingereza, Ujerumani, Ufaransa, Ubelgiji, Italia na Ureno.
B Uingereza, Ujerumani, Ufaransa, Uchina, Uhispania na Marekani.
C Uingereza, Ujerumani, Ufaransa, Japani, Uhispania na Ubelgiji.
D Uingereza, Ujerumani, Ufaransa, Urusi, Uchina na Japani.
E Uingereza, Ujerumani, Ufaransa, Ubelgiji, Italia na Uchina.

**Jedwali Na. 8: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

| Machaguo | A* | B | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 591,708 | 111,056 | 104,572 | 72,487 | 51,513 | 6,659 |
| Asilimia ya Watahiniwa | 63.08 | 11.84 | 11.15 | 7.73 | 5.49 | 0.71 |

Swali lilitoka katika mada ya *Uvamizi wa Wakoloni Barani Afrika tangu miaka ya 1880*. Swali lilipima uwezo wa watahiniwa kubaini mataifa makubwa ya kibepari yaliyogombania Bara la Afrika katika machaguo waliyopewa. Swali lilikuwa na kiwango kizuri cha ufaulu kwani watahiniwa 591,708 (63.08%) walichagua jibu sahihi A, *Uingereza, Ujerumani, Ufaransa, Ubelgiji, Italia na Ureno.* Watahiniwa hawa walikuwa na uelewa wa kina wa mataifa makubwa ya kibepari yaliyogombania Bara la Afrika. Hivyo, ilikuwa rahisi kwao kubaini chaguo sahihi ambalo lilikuwa na mataifa makubwa ya kibepari yaliyogombania bara la Afrika katika karne ya 19.


Pamoja na hayo, jumla ya watahiniwa 339,628 (36.21%) walichagua kipotoshi B, *Uingereza, Ujerumani, Ufaransa, Uchina, Uhispania na Marekani;* kipotoshi C, *Uingereza, Ujerumani, Ufaransa, Japani, Uhispania na Ubelgiji*; kipotoshi D, *Uingereza, Ujerumani, Ufaransa, Urusi, Uchina na Japani* na kipotoshi E, *Uingereza, Ujerumani, Ufaransa, Ubelgiji, Italia na Uchina*.

Uchaguzi wa vipotoshi hivyo umetokana na watahiniwa kutokuwa na maarifa ya kutosha katika mada ya *Uvamizi wa Kikoloni Barani Afrika tangu miaka 1880*. Hii ina maana kuwa, vipotoshi vilivyochaguliwa vilikuwa na mataifa ambayo hayakushiriki katika kuligawa Bara la Afrika. Mataifa hayo ni Uchina, Uhispania, Urusi na Japani. Marekani ni taifa ambalo lilishiriki katika mkutano wa kuligawa Bara la Afrika kama mgeni mtazamaji/ mwalikwa. Uchaguzi wa vipotoshi hivi unaweza pia kuwa ulisababishwa na watahiniwa kutokuwa na maarifa ya kutosha ya uvamizi wa Bara la Afrika toka mwaka 1880 na ushawishi wa mataifa ya Marekani, Japani, Urusi, Uhispania na Uchina katika maswala ya kisiasa, kiuchumi, kijamii na teknolojia duniani kuanzia karne ya 20 hadi sasa.

**Swali la 17**: Mwanzilishi wa kampuni ya kibiashara ya Kiingereza ya Afrika Mashariki (IBEACO) anaitwa

A David Livingstone. B Karl Peters. C Mungo Park.
D William Mackinnon. E Seyyid Said.

Swali hili lilitoka katika mada ya *Vitangulizi vya Ukoloni*. Swali liliwataka watahiniwa kubaini jina la mwanzilishi wa kampuni ya kibiashara ya Kiingereza ya Afrika Mashariki (IBEACO). Ufaulu katika swali hili ulikuwa ni wa wastani kwa sababu watahiniwa 457,513 (48.78%) waliweza kuchagua jibu sahihi D, *William Mackinnon*. Uchaguzi huu unathibitisha kwamba watahiniwa walikuwa na uelewa wa kutosha wa Wazungu na makampuni waliyoyaanzisha ambayo yalisaidia kutawaliwa kwa Bara la Afrika mnamo karne ya 19. Ufaulu wa watahiniwa katika swali hili umeoneshwa katika Chati Na. 9.




**Chati Na. 9**: *Inaonesha kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili.*

Hata hivyo, watahiniwa 177,898 (18.97%) walichagua kipotoshi B, *Karl Peters*. Uchaguzi wa kipotoshi hicho unaonesha kwamba, baadhi ya watahiniwa hawakuwa na maarifa ya kutosha ya majina ya waasisi na shughuli walizozifanya kupitia makampuni hayo katika kuanzisha ukoloni Afrika Mashariki. Kipotoshi kilichaguliwa kwa sababu ya umaarufu wa Karl Peters miongoni mwa watahiniwa hasa jinsi alivyosaidia kutawaliwa kwa Tanganyika kupitia mikataba ya ulanghai aliyoifanya na machifu kama vile Mangungo wa Msowero.

Aidha, watahiniwa 121,101 (12.91%) walichagua kipotoshi A, *David Livingstone*. Watahiniwa hawa walichagua kipotoshi hicho kwa sababu ya umaarufu wa David Livingstone katika Afrika Mashariki na Kati. Ukweli ni kwamba, watahiniwa hao walishindwa kutofautisha aina za vitangulizi vya ukoloni ambavyo ni wapelelezi/wamisionari na wale ambao walikuwa wafanyabiashara. Watahiniwa hawa walipaswa kufahamu kwamba, David Livingstone hakuwa mfanyabiashara na hakuasisi kampuni ya kibiashara kwani alikuwa na kazi mbili za umisionari na upelelezi.

Jumla ya watahiniwa 95,297(10.16%) walichagua kipotoshi C, *Mungo Park*. Watahiniwa hawa inawezekana hawakuwa na maarifa ya kutosha katika mada ya *Vitangulizi vya Ukoloni* na hivyo kushindwa kutofautisha makundi ya vitangulizi vya ukoloni, shughuli walizofanya na mahali walipozifanyia shughuli zao. Watahiniwa hawa walipaswa kufahamu kuwa Mungo Park alikuwa mpelelezi huko Afrika Magharibi na wala sio Afrika Mashariki.

Kipotoshi E, *Seyyid Said* kilichaguliwa na watahiniwa 78,529 (8.37%). Watahiniwa hawa hawakuwa na maarifa ya kutosha ya biashara ya watumwa na vitangulizi vya ukoloni. Watahiniwa hao walishindwa kufahamu kwamba Seyyid Said hakuwa mtangulizi wa wakoloni bali ni Sultani wa Omani aliyehamisha makao yake makuu kutoka Muscat kwenda Zanzibar mwaka 1840. Uchaguzi huu unawezakana ulisababishwa na umaarufu wa Seyyid Said kwa jinsi alivyowezesha biashara ya utumwa kushamiri Afrika Mashariki. Inapaswa kukumbuka kuwa Sultan hakuwa mmojawapo wa vitangulizi vya ukoloni katika Afrika ya Mashariki wala hakuanzisha kampuni yoyote katika Afrika ya Mashariki.

**Swali la 18:** Julius Von Soden alikuwa nani?

A Gavana wa kwanza wa Kiingereza katika Tanganyika
B Gavana wa kwanza wa Kijerumani katika Tanganyika
C Gavana wa mwisho wa Kijerumani katika Tanganyika
D Gavana wa mwisho wa Kiingereza katika Tanganyika
E Gavana aliyeanzisha utawala wa moja kwa moja katika Tanganyika

**Jedwali Na. 9: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

| Machaguo | A | B* | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 217,155 | 391,965 | 94,605 | 68,044 | 156,673 | 9,553 |
| Asilimia ya Watahiniwa | 23.15 | 41.79 | 10.09 | 7.25 | 16.70 | 1.02 |

Swali hili lilitoka katika mada ya *Kuanzishwa kwa Utawala wa Kikoloni katika Tanganyika na Zanzibar.* Swali liliwataka watahiniwa kubaini cheo cha Julius Von Soden katika koloni la Tanganyika. Kiwango cha kufaulu kwa ujumla kilikuwa ni wastani kwani watahiniwa 391,965 (41.79%) waliweza kuchagua jibu sahihi B, *Gavana wa kwanza wa Kijerumani katika Tanganyika*. Watahiniwa hao walikuwa na ufahamu wa kutosha katika mada ya *Kuanzishwa kwa Utawala wa Kikoloni katika Tanganyika na Zanzibar*. Hivyo, watahiniwa hao waliweza kubaini majina ya maofisa wa kikoloni, nchi walizotoka na mtitiriko wa uongozi wao katika Tanganyika.

Kipotoshi A, *Gavana wa kwanza wa Kiingereza katika Tanganyika* kilichaguliwa na watahiniwa 217,155 (23.15%) ambao hawakuwa na maarifa ya kutosha ya historia ya Wajerumani na Waingereza katika Tanganyika. Watahiniwa hawa walipaswa kufahamu kwamba gavana wa kwanza wa Kiingereza katika Tanganyika alikuwa Horace Byatt kuanzia mwaka 1920 hadi 1924 na sio Julius Von Soden - gavana wa Kijerumani aliyetawala Tanganyika tangu mwaka 1891 hadi 1893. Uchaguzi wa kipotoshi hicho unathibitisha kwamba watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha ya majina na vipindi mbalimbali vya watawala wa kikoloni katika Tanganyika. Watahiniwa walipaswa kufahamu kwamba, miaka sita baada ya mkutano wa Berlin; Gavana wa kwanza wa Kijerumani katika Tanganyika alikuwa Julius Von Soden.

Kipotoshi kingine kilichowavutia watahiniwa wengi 156,673 (16.70%) kilikuwa E, *Gavana aliyeanzisha utawala wa moja kwa moja katika Tanganyika*. Kwa ujumla, watahiniwa waliochagua kipotoshi hiki hawakuwa na ufahamu kuhusu magavana wa kikoloni, mihura yao na kazi walizozifanya Tanganyika katika kipindi cha ukoloni.

Kipotoshi C, *Gavana wa mwisho wa Kijerumani katika Tanganyika* kilichaguliwa na watahiniwa 94,605 (10.09%). Watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha ya utawala wa Kijerumani katika Tanganyika. Kwa ujumla, watahiniwa walipaswa kufahamu kuwa gavana wa mwisho wa Kijerumani katika Tanganyika ni Heinrich Von Schene kuanzia mwaka 1912 hadi 1917 na siyo Julius Von Soden aliyetawala koloni la Tanganyika kuanzia mwaka 1891 hadi 1893.

Watahiniwa waliochagua kipotoshi D, *Gavana wa mwisho wa Kiingereza katika Tanganyika* walikuwa 68,044 (7.25%). Watahiniwa hao walishindwa kuelewa kwamba Richard Turnbull alikuwa gavana wa mwisho wa Kiingereza katika Tanganyika na sio Julius Von Soden.

**Swali la 19:** Mtaalamu wa mambo ya kale aliyevumbua fuvu la binadamu wa kwanza Olduvai Gorge aliitwa


A Charles Darwin. B Zinjathropus. C Homo Habilis.
D David Livingstone. E Louis Leakey.

Swali lilitoka katika mada ya *Chimbuko na Mabadiliko ya Binadamu*. Swali liliwataka watahiniwa kubaini jina la mtaalamu wa mambo ya kale aliyevumbua fuvu la binadamu wa kwanza Olduvai Gorge. Ufaulu wa jumla katika swali hili ulikuwa ni wa wastani kwani watahiniwa 559,107 (59.61%) waliweza kuchagua jibu sahihi E, *Louis Leakey* ambaye ndiye mvumbuzi wa fuvu (Zinjanthropus) hilo katika mwaka 1959.

Hata hivyo, watahiniwa 136,503 (14.55%) walichagua kipotoshi A, *Charles Darwin*. Uchaguzi wa kipotoshi hiki unaweza kuwa umesababishwa na umaarufu wake miongoni mwa watahiniwa kwani ndiye mwanasayansi aliyeeleza hatua mbalimbali za mabadiliko ya binadamu. Hivyo, kwa kuwa kuna uhusiano kati ya hatua mbalimbali za mabadiliko ya binadamu na fuvu la mtu wa kale (Zinjanthropus) baadhi ya watahiniwa walifikiri kuwa Charles Darwin ndiye mvumbuzi wa fuvu hilo.

Aidha, watahiniwa 102,310 (10.91%) walichagua kipotoshi D, *David Livingstone*. Uchaguzi wa kipotoshi hiki inawezekana ulisababishwa na uelewa mdogo wa watahiniwa kuhusu *Chimbuko na Mabadiliko ya Binadamu* na vitangulizi vya wakoloni. Watahiniwa hawa walishindwa kuelewa kwamba David Livingstone hakuhusika katika uvumbuzi wa fuvu la binadamu wa kwanza bali alikuwa ni miongoni mwa kundi la watangulizi wa ukoloni walioasisi kutawaliwa kwa Bara la Afrika mnamo karne ya 19.

Kipotoshi B, *Zinjathropus* kilichaguliwa na watahiniwa 82,292 (8.77%) na wengine 50,940 (5.43%) walichagua kipotoshi C *Homo Habilis*. Watahiniwa hawa hawakuwa na maarifa ya kutosha katika mada ya *Chimbuko na Mabadiliko ya Binadamu* kwani Zinjanthropus na Homo Habilis hawakuwa wataalam wa mambo ya kale bali yalikuwa ni mafuvu ya watu wa kale yaliyovumbuliwa Olduvai Gorge na Dr. Louis Leakey katika mwaka 1959 na 1964 mtawalia.




**Chati Na. 10**: *Inaonesha kufaulu kwa kiwango cha wastani (59.61%) kwa watahiniwa waliofanya swali hili.*

**Swali la 20:** Ni lini binadamu alianza kuchoma misitu ili kuwafukuza wanyama wakali?

A Wakati wa Zama za Chuma
B Wakati wa Zama za Mwanzo za Mawe
C Wakati wa Zama za Kale za Mawe
D Wakati wa Zama za Mwisho za Mawe

E Wakati wa Zama za Kati za Mawe

**Jedwali Na. 10: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

| Machaguo | A | B | C | D | E* | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 89,131 | 72,169 | 72,366 | 190,825 | 505,619 | 7,885 |
| Asilimia ya Watahiniwa | 9.50 | 7.69 | 7.71 | 20.34 | 53.90 | 0.84 |

Swali lilitoka katika mada ya *Hatua za Maendeleo ya Binadamu katika Zama Mbalimbali*. Swali lilimtaka mtahiniwa kubaini zama ambazo binadamu alianza kuchoma misitu ili kuwafukuza wanyama wakali. Ufaulu wa swali hili ulikuwa wa wastani kwani watahiniwa 505,619 (53.90%) waliweza kuchagua jibu sahihi E, *Wakati wa Zama za Kati za Mawe*. Watahiniwa hawa walielewa kwamba moto ulimsaidia mwanadamu kulala wakati wa usiku kwani wanyama pori waliuogopa. Aidha, ulikuwa ni moto ulioondoa kikwazo cha giza na kuanza kupunguza hofu ya mwanadamu wakati wa usiku. Kwa ujumla, moto ulisafisha misitu na pia ulitumika kama tochi kuondoa giza la kutisha ambamo wanyama pori walijificha.

Jumla ya watahiniwa 190,825 (20.34%) walivutiwa na kipotoshi D, *Wakati wa Zama za Mwisho za Mawe*. Kipotoshi hiki kilivuta watahiniwa wengi kwa sababu walishindwa kutofautisha maendeleo mbalimbali ya kijamii na kiuchumi yaliyofikiwa na binadamu katika zama mbalimbali za mawe. Watahiniwa hawa walipaswa kufahamu kwamba katika kipindi cha zama za mawe za mwisho moto ulikuwa tayari umegunduliwa na binadamu tayari alianza kutumia moto sio tu kuchoma moto misitu ili kuwafukuza wanyama wakali lakini pia alitumia kupika chakula chake. Mafanikio makubwa katika michoro ya mapangoni, kilimo na ufugaji, mgawanyo wa kazi na maendeleo ya lugha katika zama hizo inawezekana kuwa ndivyo vilivyowavuta watahiniwa kuchagua kipotoshi hiki. Kiuhalisia, watahiniwa hao walishindwa kutambua mafanikio ya binadamu katika zama za mawe husika hasa kijamii, kiuchumi na kiteknolojia.

Watahiniwa waliochagua kipotoshi B, *Wakati wa Zama za Mwanzo za Mawe* na C *Wakati wa Zama za Mawe za Kale* hawakuwa na ufahamu wa maendeleo ya kiuchumi na teknolojia katika zama hizo. Watahiniwa walipaswa kufahamu kwamba zama za mawe za kale na zama za mawe za mwanzo zinatumika sawia kufafanua kipindi cha miaka kuanzia 1,750,000 KK hadi 750,000 KK. Vilevile, katika kipindi hiki binadamu aliweza kutengeneza zana za kuchimbia na kukatia. Hivyo, uchaguzi wa kipotoshi hiki unathibitisha kwamba watahiniwa hawakuwa na maarifa ya kutosha ya mafanikio katika zama za mawe.

Zaidi ya hapo, jumla ya watahiniwa 89,131 (9.50%) walichagua kipotoshi A, *Wakati wa Zama za Chuma*. Watahiniwa hawa walishindwa kutofautisha maendeleo ya binadamu na mafanikio yake katika zama mbalimbali.

**Swali la 21 :** Ni katika mfumo upi wa kiuchumi ambamo njia kuu za uzalishaji mali zilimilikiwa na wanajamii wote?

A Utumwa B Ukabaila C Ubepari
D Ujima E Ujamaa

**Jedwali 11: Idadi na wastani wa watahiniwa katika kila chaguo**

| Machaguo | A | B | C | D* | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 94,517 | 313,956 | 188,948 | 183,797 | 123,929 | 32,848 |
| Asilimia ya Watahiniwa | 10.08 | 33.47 | 20.14 | 19.59 | 13.21 | 3.50 |

Swali lilitoka katika mada ya *Kukua kwa Mifumo ya Kiuchumi na Kiutawala Katika Jamii za Kitanzania hadi Karne ya 19*. Swali lilipima uwezo wa watahiniwa kubaini mfumo wa kiuchumi ambamo njia kuu za uzalishaji mali zilimilikiwa na wanajamii wote. Ufaulu katika swali hili ulikuwa ni dhaifu kwani watahiniwa 183,797 (19.59%) tu ndio walioweza kuchagua jibu sahihi D, *Ujima*. Watahiniwa hawa walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu *kukua kwa mifumo ya kiuchumi na kiutawala katika jamii za Kitanzania kabla ya ukoloni*.

Kipotoshi B, *Ukabaila* kilichaguliwa na watahiniwa 313,956 (33.47%) ambao walishindwa kutofautisha kati ya ujima na ukabaila. Watahiniwa hawa walipaswa kufahamu kuwa katika mfumo wa ukabaila ardhi ilimilikiwa na watu wachache katika jamii. Pia, ukabaila ulikuwa na matabaka na unyonyaji kwani tabaka la makabaila lililinyonya tabaka la wasio na ardhi (vibarua).

Kipotoshi C, *Ubepari* kilichaguliwa na watahiniwa 188,948 (20.14%) ambao hawakuwa na maarifa ya kutosha ya sifa za mfumo wa ubepari. Watahiniwa hawa walipaswa kufahamu kuwa katika ubepari njia kuu za uzalishaji mali hazikumilikiwa na wanajamii wote na badala yake njia kuu za uzalishaji mali kama vile viwanda zilimilikiwa na watu wachache wakati watu wengi hawakumiliki chochote zaidi ya nguvukazi.

Vilevile, watahiniwa 123,929 (13.21%) waliochagua kipotoshi E, *Ujamaa* walikuwa na uelewa mdogo wa mada. Watahiniwa hawa walipaswa kuelewa kwamba ujamaa ni mfumo wa kisiasa na kiuchumi uliojengwa juu ya misingi ya usawa katika ugawanaji wa mali na dola ndiyo yenye mamlaka ya kumiliki njia kuu zote za uchumi.

Kipotoshi A, *Utumwa* kilivuta watahiniwa 94,517 (10.08%) ambao walikosa maarifa ya sifa za mifumo ya uzalishaji mali. Watahiniwa walipaswa kufahamu kwamba katika mfumo wa utumwa binadamu alimilikiwa na kutumiwa kama zana ya kuzalisha mali, hivyo hakukuwa na uwezekano wa watumwa kuwa ni sehemu ya wanajamii inayomiliki njia kuu za uzalishaji mali.


**Swali la 22:** Kama Juma na Hawa ni watoto wa Masanja Muntente, je, Hawa anamwitaje Juma?

A Binamu B Mjomba C Shemeji
D Mpwa E Kaka

Swali hili lilitoka katika mada ya *Familia Yetu* na lilipima uwezo wa watahiniwa kubaini namna Juma na Hawa ambao wote ni watoto katika familia ya Masanja Muntente wanavyohusiana. Ufaulu katika swali hili ulikuwa ni mzuri kwani watahiniwa 755,702 (80.57%) waliweza kuchagua jibu sahihi E, *Kaka*. Watahiniwa hao walielewa

majina ya wanafamilia hivyo walifahamu kuwa mwanaume ambaye mmezaliwa naye kwa baba na mama anaitwa kaka. Uchaguzi wa jibu sahihi unaweza kuwa ulisababishwa na uwezo wa watahiniwa kuhawilisha maarifa kutoka katika familia au mazingira wanazoishi.

Hata hivyo, jumla ya watahiniwa 174,440 (18.60%) walichagua vipotoshi A, *Binamu*; B, *Mjomba*; C, *Shemeji* na D, *Mpwa*. Uchaguzi wa vipotoshi hivi unaweza kuwa ulisababishwa na watahiniwa kutokuwa na ufahamu wa kutosha wa mada ya Familia Yetu na pia kushindwa kuhawilisha maarifa kutoka mazingira wanayoishi.





**Chati Na. 11**: *Inaonesha kufaulu kwa kiwango kizuri (80.57%) kwa watahiniwa waliofanya swali*

**Swali la 23:** Binti wa shangazi yako huitwa

| | | |
|---|---|---|
| A mpwa | B binamu | C Mama mkwe |
| D shemeji | E dada | |

Swali liliwataka watahiniwa kubaini jina la mahusiano la mtoto wa kike wa shangazi. Ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri kwani watahiniwa 683,880 (72.91%) waliweza kuchagua jibu sahihi B, *binamu*. Watahiniwa hawa walielewa kuwa watoto wa mjomba au shangazi wanaitwa binamu. Pia, watahiniwa waliweza kuchagua jibu sahihi kutokana na uwezo wa watahiniwa kuhawilisha maarifa

kutoka katika familia au mazingira yao. Hata hivyo, jumla ya watahiniwa 247,984 (26.44%) walichagua vipotoshi A, *mpwa*; C, *Mama mkwe*; D, *shemeji*; na E, dada. Uchaguzi wa vipotoshi hivyo unaonesha kwamba watahiniwa hao hawakuwa na ufahamu wa kutosha wa majina ya mahusiano katika familia.




**Chati Na. 12**: *Inaonesha kufaulu kwa kiwango kizuri (72.91%) kwa watahiniwa waliofanya swali.*

**Swali la 24 :** Kwa nini vita vya Maji Maji vilitokea?

A Wareno waliwapeleka Watanganyika utumwani

B Kinjekitile alikasirishwa na uhasama wa Wajerumani na Waarabu

C Watanganyika walipigwa mijeledi na Waingereza

D Wajerumani waliwalazimisha watu kufanya kazi katika mashamba ya pamba

E Sultan Seyyid Said aliwatesa na kuwatumikisha Waafrika

Swali liliwataka watahiniwa kubaini sababu ya kutokea kwa vita vya Maji Maji. Ufaulu katika swali hili ulikua ni wa wastani kwani watahiniwa 415,982 (44.35%) waliweza kuchagua jibu sahihi D, *Wajerumani waliwalazimisha watu kufanya kazi katika mashamba ya pamba*. Watahiniwa hao walitambua kwamba vita vya majimaji ni

mojawapo ya upinzani maarufu wa Waafrika dhidi ya unyonyaji na ukandamizaji wa utawala wa Kijerumani katika Tanganyika.


Hata hivyo, watahiniwa 297,319 (31.70%) walichagua kipotoshi B, *Kinjekitile alikasirishwa na uhasama wa Wajerumani na Waarabu*. Watahiniwa hao pengine walivutiwa na umaarufu wa Kinjeketile Ngwale ambaye alikuwa ni mtaalamu wa tiba za jadi aliyetumia mbinu ya dawa ya jadi ya maji kuwahamasisha watu wa Kusini mwa Tanganyika kupinga utawala wa Wajerumani. Katika muktadha huu, watahiniwa hao walipaswa kufahamu kwamba sababu ya Kinjeketile Ngwale kukasirishwa na uhasama wa Wajerumani na Waarabu haikuwa na ukweli wowote kwani uhasama kati ya Wajerumani na Waarabu haukuwa na uhusiano na kutokea kwa vita vya Maji Maji.

Kipotoshi E, *Sultan Seyyid Said aliwatesa na kuwatumikisha Waafrika* kilichaguliwa na watahiniwa 82,572 (8.80%) ambao walishindwa kuelewa kuwa Sultan Seyyid Said hakuhusika na kuibuka kwa Vita vya Maji Maji kwani Sultan Seyyid Said alifariki miaka 49 (mwaka 1856) kabla ya kutokea vita vya Maji Maji. Kwa kifupi, watahiniwa walipaswa kuelewa kwamba Sultan Seyyid Said alikuwa ni mawala aliyehamisha makao yake kutoka Muscat Oman kuja Zanzibar mwaka 1840 kwa lengo la kuanzisha mashamba ya karafuu na nazi na pia kudhibiti biashara ya watumwa katika bahari ya Hindi. Kwa hiyo, athari yake ilimalizika alipofariki mwaka 1856.

Kipotoshi C, *Watanganyika walipigwa mijeledi na Waingereza* kilichaguliwa na watahiniwa 68,931 (7.35%) walioshindwa kufahamu kuwa Tanganyika lilikuwa koloni la Wajerumani tangu 1890 hadi mwaka 1918 na baadae Waingereza walilitawala hadi mwaka 1961. Kwa hiyo, watahiniwa hao walipaswa kuelewa kuwa vita vya majimaji vilitokea kuanzia mwaka 1905 hadi 1907 wakati Tanganyika ikiwa chini ya utawala wa Kijerumani. Hii inamaanisha kwamba vita vya majimaji vilitokea miaka kumi na mbili kabla ya utawala wa Kiingereza katika Tanganyika.

Kipotoshi A, *Wareno waliwapeleka Watanganyika utumwani* kilichaguliwa na watahiniwa 64,336 (6.86%) ambao inawezekana walichanganya maarifa ya mada ya *Upinzani Dhidi ya Uvamizi wa*

*Kikoloni Tanganyika na Zanzibar* na ile ya Uhusiano wa Jamii za Kitanzania na Jamii za Kizungu. Wareno waliondolewa katika pwani ya Afrika ya Mashariki mwaka 1698, hivyo, ni vigumu kwa athari zao kusababisha vita vya majimaji miaka zaidi ya 200 baada ya Wareno kuondoshwa.




**Chati Na. 13**: *Inaonesha kufaulu kwa kiwango cha wastani (44.35%) kwa watahiniwa waliofanya swali hili*

**Swali la 25:** Rais Julius Kambarage Nyerere na Kwame Nkrumah walikuwa

A waanzilishi wa Jumuia ya Afrika Mashariki.
B waanzilishi wa Umoja wa Mataifa.
C waanzilishi wa Jumuia ya Mataifa.
D waanzilishi wa Umoja wa Nchi huru za Kiafrika.
E waanzilishi wa Jumuia ya Madola.

Swali lilitoka katika mada ya *Ushirikiano wa Kimataifa*. Swali lilitaka kubaini uwezo wa watahiniwa kubaini michango ya Marais Julius Kambarage Nyerere na Kwame Nkrumah katika ushirikiano wa kimataifa. Swali hili lilikuwa na ufaulu wa wastani kwani watahiniwa 487,302 (51.95%) waliweza kuchagua jibu sahihi D, *waanzilishi wa Umoja wa Nchi huru za Kiafrika*. Watahiniwa hawa walikuwa na


ufahamu wa kutosha katika mada hivyo, waliweza kubaini kwamba Julius Kambarage Nyerere na Kwame Nkrumah walikuwa waasisi wa Jumuia ya Umoja wa nchi huru za Kiafrika katika miaka ya 1960 mjini Addis Ababa, Ethiopia.

Jumla ya watahiniwa 210,257 (22.42%) walichagua kipotoshi A, *waanzilishi wa Jumuia ya Afrika Mashariki*. Watahiniwa hawa walishindwa kufahamu kwamba Kwame Nkrumah alikuwa Rais wa Ghana - taifa lililoko Afrika ya Magharibi, hivyo haikuwa rahisi kwake kuhusika na uasisi Jumuia ya Afrika Mashariki.

Vilevile, watahiniwa 119,659 (12.76%) walichagua kipotoshi B, *waanzilishi wa Umoja wa Mataifa*. Ingawa watahiniwa walitambua uanachama wa mataifa ya Tanganyika na Ghana katika Umoja wa Mataifa lakini hawakufahamu kuwa Umoja wa Mataifa uliasisiwa mwaka 1945 na siyo miaka ya 1960 ambapo viongozi hawa wa Umoja wa Waafrika walikuwa viongozi katika mataifa yao. Pia, watahiniwa hao walishindwa kutofautisha Umoja wa Nchi huru za Kiafrika na Umoja wa Mataifa.

Kipotoshi E, *waanzilishi wa Jumuia ya Madola* kilivutia asilimia 6.09 ya watahiniwa. Watahiniwa hao walishindwa kufahamu kwamba Jumuia ya Madola iliasisiwa mwaka 1931, kipindi ambacho Julius Kambarage Nyerere alikuwa na umri wa miaka 9. Hivyo, Jumuia hiyo isingeweza kuasisiwa na viongozi hao. `

Baadhi ya watahiniwa 55,610 (5.93%) walichagua kipotoshi C, *waanzilishi wa Jumuia ya Mataifa*. Uchaguzi wa kipotoshi hiki unaonesha kwamba watahiniwa hawakuwa na maarifa ya kutosha katika mada ya Ushirikiano wa Kimataifa. Kinachoweza kubainika kutokana na uchaguzi huo ni kwamba watahiniwa hawakuwa na maarifa ya kutosha ya tarehe mahususi za kuasisiwa jumuia za kimataifa. Watahiniwa walipaswa kufahamu kwamba Jumuia ya Mataifa iliasisiwa mwaka 1920 mwaka ambao Julius Kambarage Nyerere alikuwa bado hajazaliwa.





**Chati Na. 14**: *Inaonesha kufaulu kwa kiwango cha wastani (51.95%) kwa watahiniwa waliofanya swali*

**Swali la 26:** Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia elimu na utamaduni linaitwa

A WHO. B UNICEF. C UNESCO.
D UNHCR. E UNDP.

Swali lilitaka kupima uwezo wa watahiniwa kubaini shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia elimu na utamaduni. Kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kilikuwa ni kizuri kwani watahiniwa 574,692 (61.27%) waliweza kuchagua jibu sahihi C, *UNESCO*. Watahiniwa hawa walikuwa na maarifa ya kutosha katika mada ya *Ushirikiano wa Kimataifa*. Kwa hiyo, watahiniwa walikuwa na ufahamu wa mashirika mbalimbali ya Umoja wa Mataifa pamoja na kazi yanazozifanya.

Hata hivyo, asilimia 37.97 ya watahiniwa walichagua vipotoshi A, *WHO;* B, *UNICEF*; E, *UNDP* na D, *UNHCR*. Watahiniwa hao walichagua vipotoshi hivi kwa sababu walishindwa kutofautisha shughuli za mashirika ya Umoja wa Mataifa.




**Chati Na. 15**: *Inaonesha kufaulu kwa kiwango kizuri (61.27%) kwa watahiniwa waliofanya swali hili.*

### 2.1.3 Kipengele III: Jiografia

**Swali la 27:** Wakati wa mvua kubwa inayoambatana na radi, watu hawashauriwi

A kuvaa nguo nyekundu.
B kutumia miavuli.
C kufungua milango na madirisha.
D kujificha chini ya mti.
E kufunga luninga na redio.

Swali hili lilitoka katika mada ya *Majanga* na watahiniwa walitakiwa kubainisha tahadhari zinazopaswa kuchukuliwa na watu wakati wa mvua kubwa inayoambatana na radi. Kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kulikuwa kwa kiwango cha wastani kwani jumla ya watahiniwa 504,694 (53.81%) waliweza kuchagua jibu sahihi *D, kujificha chini ya mti*. Watahiniwa hawa walikuwa na uelewa wa kutosha kuwa miti mara nyingi ni mirefu hivyo ni rahisi kunasa radi.

Radi ikishanaswa na mti huweza kumpiga na kusababisha kifo au kumjeruhi mtu aliyeko chini ya mti huo.


Watahiniwa waliobaki walichagua majibu yasiyo sahihi, ambapo jumla ya watahiniwa 170,801 (18.21%) walichagua *E, kufunga luninga na redio.* Watahiniwa hawa hawakuwa na ufahamu kuhusu tahadhari zinazopaswa kuchukuliwa wakati wa mvua kubwa inayoambatana na radi ambazo ni pamoja na kufunga luninga na redio na vifaa vingine vya umeme hasa katika majengo yasiyo na waya za kuzuia radi.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 141,770 (15.11%) walichagua kipotoshi *A, kuvaa nguo nyekundu* ambapo nguo nyekundu haina uhusiano wowote na r*adi.* Pia watahiniwa 60,395 (6.44%) walichagua kipotoshi *C*, *kufungua milango na madirisha*. Watahiniwa hao hawakuwa na uelewa kuhusu tahadhari tunazopaswa kuzichukua wakati wa mvua kubwa inayoambatana na radi. Aidha, watahiniwa 52,585 (5.61%) waliochagua kipotoshi *B, kutumia miamvuli* walishindwa kutofautisha mvua kubwa inayoambatana na radi na mvua ya kawaida inayoweza kuruhusu matumizi ya miavuli. Watahiniwa wengine waliobaki wapatao 7,750 sawa na asilimia 0.83 hawakujibu kabisa swali hili au walichagua jibu zaidi ya moja.

**Swali la 28:** Janga la kimazingira linalosababishwa na nguvu za asili pekee linaitwa

A ukame.
B tetemeko la ardhi.
C mmomonyoko wa udongo.
D njaa.
E uchafuzi wa mazingira.

Swali hili lilikusudia kupima uwezo wa watahiniwa kubainisha janga la kimazingira linalosababishwa na nguvu za asili pekee. Mtawanyiko wa majibu ya watahiniwa na kiwango cha kufaulu vimeoneshwa katika Chati Na. 16.




**Chati Na. 16:** *Inaonesha kiwango kizuri (67.29%) cha kufaulu kwa watahiniwa waliofanya swali hili.*

Kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kulikuwa kwa kiwango kizuri kwani jumla ya watahiniwa 631,132 (67.29%) waliweza kuchagua jibu sahihi *B, tetemeko la ardhi.* Watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mada ya majanga. Pia, watahiniwa hao walikuwa na ufahamu kuwa tetemeko la ardhi ni janga linalosababishwa na nguvu za asili kama vile milipuko ya volkano na siyo shughuli za binadamu.

Hata hivyo, jumla ya watahiniwa 302,153 (32.21%) walichagua vipotoshi *A, Ukame* (10.40%); *C, Mmomonyoko wa udongo* (10.88%); D*, Njaa (*5.90%) *na E, Uchafuzi wa mazingira (*5.03%). Watahiniwa hao hawakuwa na uelewa wa kutosha wa mada ndogo inayohusu majanga ya kimazingira yanayosababishwa na nguvu za kiasili kwani machaguo hayo yaliwakilisha majanga ya kimazingira ambayo kwa kiasi kikubwa yanasababishwa na shughuli za kibinadamu.

**Swali la 29:** Uchafuzi wa maji unaweza kuepukwa kwa

A utupaji hovyo wa taka za kemikali.

B utupaji sahihi wa majitaka.

C matumizi ya mbolea ya chumvichumvi.

D kuvua samaki kwa kutumia sumu.
E kuosha magari katika mito.

**Jedwali Na. 12: Idadi na asilimia ya watahiniwa kwa kila chaguo**

| Machaguo | A | B* | C | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 147,401 | 570,719 | 77,434 | 92,813 | 42,643 | 6,985 |
| Asilimia ya Watahiniwa | 15.71 | 60.84 | 8.26 | 9.89 | 4.55 | 0.74 |

Swali hili lilipima uelewa wa watahiniwa kuhusu mbinu za kuepuka uchafuzi wa maji. Kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kulikuwa kwa kiwango kizuri ambapo jumla ya watahiniwa 570,719 (60.84%) walichagua jibu sahihi B*, utupaji sahihi wa maji taka.* Utupaji sahihi wa maji taka hufanyika baada ya kuyawekea dawa ya kuua vijidudu vya magonjwa na chemikali zingine ili yaweze kutumika kwa matumizi mengine kama vile shughuli za umwagiliaji. Badala ya kuyaacha maji taka yasambae hovyo na kuchafua vyanzo vingine vya maji.

Hata hivyo, jumla ya watahiniwa 360,291 (38.41%) walichagua majibu yasiyo sahihi *A, utupaji hovyo wa taka za kemikali (*15.71%)*; C, matumizi ya mbolea ya chumvichumvi (*8.26%)*; D, kuvua samaki kwa kutumia sumu (*9.89%) *na E, kuosha magari katika mito (*4.55%). Watahiniwa hao hawakuwa na uelewa wa kutosha wa mada inayohusu *Utunzaji wa Maji* kwani walichagua majibu yanayosababisha uchafuzi wa maji kinyume cha matakwa ya swali.


**Swali la 30:** Upi ni mlingano sahihi wa viumbe hai?

A Swala → simba → nyasi.
B ng'ombe → swala → nyasi.
C Nyasi → simba → swala.
D swala → nyasi → simba.
E Simba → swala → nyasi.

Swali hili lilitungwa kutoka katika mada ya *Kutegemeana katika Mazingira* na lilipima uwezo wa watahiniwa kuonesha jinsi viumbe

hai wanavyotegemeana katika mazingira. Kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kulikuwa kwa kiwango kizuri kwani jumla ya watahiniwa 668,770 (71.30%) walichagua jibu sahihi *E, Simba* ***hula*** *swala* ***hula*** *nyasi*. Watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa kutosha wa jinsi viumbe hai vinavyotegemeana hivyo waliweza kutambua kwa urahisi mlingano sahihi uliopo kati yao ambapo mnyama simba anaishi kwa kula nyama (swala) na swala anaishi kwa kula majani (nyasi).

Hata hivyo, jumla ya watahiniwa 260,697 (27.79%), walichagua vipotoshi *A, Swala* ***hula*** *simba* **hula** nyasi (6.19%); *B, ng'ombe* ***hula*** *swala* ***hula*** *nyasi* (10.24%); *C, nyasi* ***hula*** *simba* ***hula*** *swala* (5.44%) na *D, swala* ***hula*** *nyasi* ***hula*** *simba* (5.92%). Machaguo hayo yanaashiria kuwa watahiniwa hao hawakuwa na ufahamu wa kutosha kuhusu mlingano uliopo kati ya viumbe hai kwani walishindwa kutambua kuwa baadhi ya wanyama hawali wanyama wenzao. Kwa mfano; swala hawezi kumla simba na ng'ombe hawezi kumla swala. Kwa upande mwingine, watahiniwa hao walishindwa kutambua kuwa baadhi ya wanyama hawali nyasi kwa mfano; simba hali nyasi pia hawezi kuliwa na nyasi. Kufaulu kwa watahiniwa kumeoneshwa katika Chati Na. 17.




**Chati 17:** *Inaonesha kiwango kizuri (71.30%) cha kufaulu kwa watahiniwa.*

**Swali la 31:** Zifuatazo ni njia bora za kutunza mazingira **isipokuwa**

A kudhibiti uchafuzi wa hewa.
B kilimo cha kuhamahama.
C kuthibiti takataka za viwandani.
D kupanda miti.
E kutunza vyanzo vya maji.

Swali hili lilitungwa kutoka katika mada ya *Mazingira* na lilipima uwezo wa watahiniwa kubainisha chaguo ambalo si njia bora katika utunzaji wa mazingira.

Kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kilikuwa kizuri ambapo jumla ya watahiniwa 697,283 (74.34%) waliweza kuchagua jibu sahihi *B, kilimo cha kuhamahama.* Watahiniwa hao walikuwa na uelewa sahihi kuhusu kilimo cha kuhamahama ambacho kinahusisha uhamishaji wa shughuli ya kilimo kutoka sehemu moja kwenda nyingine baada ya ardhi kupoteza rutuba. Kilimo hiki kinaambatana na ukataji hovyo wa miti ambao ni chanzo kikuu cha uharibifu wa mazingira. Hivyo, walitambua kwamba kilimo cha kuhamahama sio njia bora ya kutunza mazingira.


Hata hivyo, jumla ya watahiniwa 234,354 (24.98%) walichagua majibu yasiyo sahihi *A, kudhibiti uchafuzi wa hewa* (6.67%); *C, kuthibiti takataka za viwandani* (8.64%); D*, kupanda miti* (5.51%) *na E, kutunza vyanzo vya maji (*4.16%). Watahiniwa hao hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mbinu bora za utunzaji wa mazingira kwani machaguo hayo yote yanahusisha njia bora za utunzaji wa mazingira. Pia watahiniwa hawa walishindwa kuyahusisha majibu yao na matakwa ya swali au hawakubaini matumizi ya neno "*isipokuwa"* katika swali. Watahiniwa wengine waliobaki wapatao 6,358 sawa na asilimia 0.68 hawakujibu kabisa swali hili au walichagua jibu zaidi ya moja.

**Swali la 32:** Kipi kati ya vipimio vya ramani vifuatavyo kinawakilisha eneo dogo?

A 1:50 B 1:500,000 C 1:50,000
D 1:5,000 E 1:500

Swali lilitoka katika mada ya *Stadi za Ramani.* Watahiniwa walitakiwa kubaini uhusiano uliopo kati ya vipimio vya ramani na umbali katika eneo halisi. Kwa ujumla kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kulikuwa kwa kiwango hafifu kwani ni watahiniwa 217,779 (23.22%) tu ambao ni pungufu ya robo ya watahiniwa wote waliofanya mtihani, waliweza kuchagua jibu sahihi *A, 1:50.* Watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu aina mbalimbali za vipimio vya ramani na matumizi yake hivyo ilikuwa rahisi kwao kuchagua kipimio kinachowakilisha eneo dogo na lenye vitu vingi.

Kwa upande mwingine, jumla ya watahiniwa 507,573 (54.11%) waliochagua *B, 1:500,000* walishindwa kutambua kuwa hicho ni kipimio kidogo cha ramani ambacho kinatumika kuwakilisha eneo kubwa la ardhi kama vile nchi, bara au dunia tofauti na matakwa ya swali. Watahiniwa 101,097 (10.78%) walichagua *C*, *1:50,000* ambacho ni kipimio cha kati kinachotumika kuwakilisha eneo lenye ukubwa wa wastani. Watahiniwa 59,895 (6.39%) walichagua *D, 1:5,000* na 44,711 (4.77%) walichagua *E, 1:500* ambavyo vyote vinatumika kuwakilisha eneo dogo lakini si dogo sawa na lile linalowakilishwa na kipimio kilichopo katika jibu sahihi. Kufaulu kwa watahiniwa kumeoneshwa katika Chati Na.18.





**Chati Na. 18:** *Inaonesha kiwango hafifu (23.22%) cha kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili.*

**Swali la 33:** Milima mikunjo hutokea katika maeneo yenye

A miamba tabaka.
B miamba volcano na moto.
C miamba geu.
D miamba moto.
E miamba volkano.

Swali hili lilitungwa kutoka katika mada ya *Mazingira.* Watahiniwa walitakiwa kubaini miamba ambayo milima mikunjo hutokea. Kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kulikuwa kwa kiwango hafifu kwani watahiniwa 218,184 (23.26%) tu waliweza kuchagua jibu sahihi *A, miamba tabaka.* Watahiniwa hao walikuwa na ufahamu wa kutosha kwamba milima mikunjo hutokea katika maeneo yenye miamba tabaka ambayo huruhusu mikunjo kutokea baada ya kukutana na nguvu ya mgandamizo. Kufaulu kwa watahiniwa kumeoneshwa katika Chati Na. 19.




**Chati Na. 19:** *Inaonesha kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kuwa ni kwa kiwango hafifu.*

Kwa upande mwingine watahiniwa 709,649 ambao ni sawa na asilimia 75.66 walikwenda kinyume cha matakwa ya swali kwani walichagua majibu yasiyo sahihi kama ifuatavyo*: B, miamba ya volcano na moto (16.96%); C, miamba* geu *(35.22%)*; *D, miamba moto (9.52%) na E, miamba volkano (13.96%).* Watahiniwa hao walishindwa kutambua kwamba miamba mingine kama vile moto na geu ina sifa ya ugumu, hivyo haiwezi kujikunja baada ya kukutana


na nguvu ya mgandamizo badala yake huvunjika. Pia, miamba ya volkano hutokana na milipuko ya volkano.

**Swali la 34:** Angahewa lina sehemu kuu ngapi?

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| A | Nne | B | Nane | C | Mbili |
| D | Tatu | E | Tano | | |

Swali lililenga kupima uwezo wa watahiniwa kubaini sehemu kuu za angahewa. Kufaulu kwa ujumla kwa watahiniwa katika swali hili kulikuwa kwa kiwango hafifu kwani ni watahiniwa 193,063 (20.58%) tu ambao ni pungufu ya robo ya watahiniwa wote waliofanya swali hili, waliweza kuchagua jibu sahihi *A, Nne.* Watahiniwa hao walikuwa na ufahamu wa kutosha kuhusu angahewa na sehemu zake kuu nne ambazo ni tabakatropo (troposphere), tabakastrato (stratosphere), tabakakati (mesosphere) na tabakajoto (thermosphere).

Hata hivyo, watahiniwa 734,326 ambao ni sawa na asilimia 78.29 walichagua vipotoshi, *B, C, D na E* kama ifuatavyo*: B, Nane (*9.38%)*; C, mbili (*33.89%); *D, Tatu (*27.00%) *na E, Tano (*8.02%) ambayo hayakuwa sahihi*.* Uchaguzi wa vipotoshi hivyo unaonesha ufinyu wa maarifa waliokuwa nayo watahiniwa kuhusiana na sehemu kuu za angahewa. Kufaulu kwa watahiniwa kumeoneshwa katika Chati Na. 20.




**Chati Na. 20:** *Inaonesha kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kulikuwa kwa kiwango hafifu (20.58%).*

**Swali la 35:** Vifuatavyo ni vipengele vinavyounda hali ya hewa **isipokuwa**

A mvua. B unyevu. C upepo.
D mwanga wa jua. E udongo.

Swali hili lilitoka katika mada ya *Hali ya Hewa.* Watahiniwa walitakiwa kubainisha chaguo ambalo si kipengele cha hali ya hewa. Kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kulikuwa kwa kiwango kizuri kwani watahiniwa 695,860 ambao ni sawa na asilimia 74.19 waliweza kuchagua jibu sahihi *E, udongo.* Hali hii inaonesha kuwa watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu vipengele vinavyounda hali ya hewa hivyo waliweza kutofautisha vipengele hivyo na kile ambacho sicho. Udongo siyo kipengele kinachounda hali ya hewa bali ni tabaka la juu la ardhi ambalo mimea huota na vipengele vya hali ya hewa vinapatikana kuanzia uso wa dunia kwenda katika anga.

Kwa upande mwingine, asilimia 25.81 ya watahiniwa hawakuelewa matakwa ya swali. Kwa mfano, watahiniwa 87,747 ambao ni sawa na asilimia 9.35 walichagua *D, mwanga wa jua*; 58,646 sawa na asilimia 6.25 walichagua *B, unyevu*; 50,063 sawa na asilimia 5.34 walichagua *C, upepo* na watahiniwa 38,960, sawa na asilimia 4.15 walichagua *A, mvua*. Machaguo hayo yote ni vipengele vinavyounda hali ya hewa tofauti na matakwa ya swali. Watahiniwa 6,719 (0.72%) hawakujibu swali hili au walichagua majibu zaidi ya moja.

**Swali la 36:** Ipi ni athari ya ongezeko kubwa la watu?

A Kupungua kwa uhalifu
B Ongezeko la ajira
C Kupungua kwa mitaji
D Kupungua kwa biashara ndogondogo
E Kutotosheleza kwa huduma za jamii

Swali hili lilitoka katika mada ya *Idadi ya Watu na Makazi*. Swali liliwataka watahiniwa wabainishe athari zinazotokana na ongezeko kubwa la watu. Kufaulu katika swali hili kulikuwa kwa kiwango cha wastani kwani watahiniwa 559,716 ambao ni sawa na asilimia 59.67 walichagua jibu sahihi *E*, *kutotosheleza kwa huduma za jamii.* Watahiniwa hao walielewa kuwa watu wanahitaji huduma za jamii

kama vile maji, umeme, matibabu na elimu. Hivyo, ongezeko la watu linapokuwa kubwa mahitaji ya huduma hizo pia yanakuwa makubwa. Ikiwa mipango mikakati haitachukuliwa kulingana na ongezeko hilo huduma hizo hazitatosheleza.

Watahiniwa wengine (40.33%) hawakuelewa vizuri mada ndogo juu ya athari za *Ongezeko Kubwa la Watu*. Kwa mfano, watahiniwa 124,211 ambao ni sawa na asilimia 13.24 walichagua *B, ongezeko la ajira*. Watahiniwa hawa walishindwa kubaini kuwa ongezeko la ajira si athari ya ongezeko kubwa la watu, bali ni kinyume chake. Ongezeko kubwa la watu husababisha uhaba wa ajira kutokana na ongezeko la ushindani katika soko la ajira.

Vilevile, watahiniwa 109,427 (11.67%) walichagua kipotoshi *C, kupungua kwa mitaji*; 77,124 sawa na asilimia 8.22 walichagua kipotoshi *D, kupungua kwa biashara ndogondogo* na watahiniwa, 59,694 sawa na asilimia 6.36 ya watahiniwa walichagua kipotoshi *A, kupungua kwa uhalifu*. Watahiniwa hawa walishindwa kutambua kuwa ongezeko kubwa la watu husababisha ongezeko la uhalifu, ongezeko la biashara ndogondogo, kupungua kwa ajira na mitaji. Watahiniwa wengine waliobaki wapatao 7,823 sawa na asilimia 0.83 hawakujibu kabisa swali hili au walichagua jibu zaidi ya moja.

**Swali la 37:** Tatizo kubwa linalowakabili wakulima wengi wa Afrika Mashariki ni pamoja na

A uwepo wa mvua nyingi mwaka mzima.
B mvua zisizoaminika.
C uwepo wa masoko ya uhakika.
D uhaba wa maeneo ya kulima.
E matumizi ya mbolea za chumvi.

Swali hili lilitoka katika mada ya *Shughuli za Kiuchumi Afrika Mashariki na Athari Zake kwenye Mazingira.* Kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kulikuwa kwa kiwango cha wastani kwani watahiniwa 430,093 ambao ni sawa na asilimia 45.85 walichagua jibu sahihi *B*, *mvua zisizoaminika.* Watahiniwa hawa walikuwa na uelewa wa kutosha kuwa shughuli za kilimo zinazofanyika katika

nchi zinazounda Afrika Mashariki zinategemea mvua. Mvua hizo zikiwa siyo za kuaminika zinasababisha shughuli za kilimo kutofanyika kwa ufasaha.

Watahiniwa wengine sawa na asilimia 54.15 ya watahiniwa wote walionesha kutoelewa matakwa ya swali. Watahiniwa hao hawakuzingatia matumizi ya neno 'kubwa' ambalo limetumika kwenye swali hilo hivyo kuchagua chaguzi ambazo zilibainisha ukweli wa kuwepo kwa matatizo lakini matatizo hayo si makubwa. Kwa mfano, watahiniwa 211,179 ambao ni sawa na asilimia 22.51 walichagua kipotoshi *D, uhaba wa maeneo ya kulima*, ambalo ni kweli ni moja ya matatizo yanayokabili wakulima katika maeneo machache ya Rwanda, Kenya na baadhi ya maeneo hapa Tanzania hasa mkoa wa Kilimanjaro, lakini katika maeneo mengine kama vile Kigoma, Morogoro, Rukwa na Ruvuma ardhi si tatizo. Hivyo basi uhaba wa ardhi si tatizo kubwa ukilinganisha na 'mvua zisizoaminika'.

Aidha, katika machaguo mengine yaliyobaki *A, uwepo wa mvua nyingi mwaka mzima* kiliwavuta watahiniwa wapatao 126,454 ambao ni sawa na asilimia 13.48. Ni kweli kuna maeneo machache yanapata mvua nyingi kama vile mkoa wa Kagera nchini Tanzania. Pia kuna maeneo kama vile singida Dodoma na Kaskazini mwa Kenya ambako uhaba wa mvua ni mkubwa. Watahiniwa 99,298 sawa na asilimia 10.59 walichagua kipotoshi *C, uwepo wa masoko ya uhakika* na watahiniwa 63,110 sawa na asilimia 6.73 walichagua *E, matumizi ya mbolea za chumvi*. Matatizo haya ni madogo na yapo katika baadhi ya maeneo na siyo maeneo yote ya Afrika Mashariki. Watahiniwa 7,861 (0.84%) waliobaki hawakujibu swali hili au walichagua majibu zaidi ya moja.

**Swali la 38:** Shughuli inayohusisha kununua, kuuza au kubadilishana bidhaa huitwa

A uwekezaji. B ujasiriamali. C biashara.
D mitaji. E utajiri.

**Jedwali 13: Idadi na wastani wa watahiniwa katika kila chaguo**

| Chaguo | A | B | C* | D | E | Mengine |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watahiniwa | 56,193 | 202,097 | 605,152 | 44,450 | 24,256 | 5,847 |
| Asilimia ya Watahiniwa | 5.99 | 21.55 | 64.52 | 4.74 | 2.59 | 0.62 |

Swali hili lilitoka katika mada ya *Mawasiliano, Biashara na Uchukuzi.* Watahiniwa walitakiwa kubainisha shughuli inayohusisha kununua, kuuza au kubadilishana bidhaa. Kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kulikuwa kwa kiwango kizuri kwani watahiniwa 605,152 ambao ni sawa na asilimia 64.52 waliweza kuchagua jibu sahihi *C, biashara*. Watahiniwa hawa walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu maana ya neno biashara.

Aidha, chaguo *B, ujasiriamali* liliwavuta watahiniwa 202,097 ambao ni sawa na asilimia 21.55 ya watahiniwa wote waliojibu swali hili. Watahiniwa hawa walishindwa kutofautisha *ujasiliamali na biashara.* Ujasiliamali ni ujuzi na maarifa ya mtu katika kutumia fursa zilizopo kufanya kitu kipya na tofauti ili kujiletea kipato na kuleta faida katika jamii kwa ujumla. Wakati biashara ambayo ni shughuli mbalimbali zinazohusisha kununua, kuuza, au kubadilishana bidhaa. Pia, watahiniwa 56,193 sawa na asilimia 5.99 walichagua kipotoshi *A, uwekezaji*, watahiniwa 44,450 sawa na asilimia 4.74 walichagua *D, mitaji* na watahiniwa 24,256 ambao ni sawa na asilimia 2.59 walichagua *E, utajiri*. Vipotoshi hivi kwa namna moja au nyingine vinahusiana na biashara lakini havibebi maana ya neno biashara.

**Swali la 39:** Biashara ya kimataifa inahusisha.


A uingizaji na usafirishaji bidhaa nje ya nchi.
B uingizaji bidhaa toka nje ya nchi tu.
C usafirishaji bidhaa kwenda nje ya nchi tu.
D kufanya biashara kwa kutumia pesa.
E kukopa fedha kutoka nje ya nchi.

Swali hili lilitoka katika mada ya *Mawasiliano, Biashara na Uchukuzi.* Watahiniwa walitakiwa kubainisha vipengele vinavyohusisha biashara ya kimataifa. Kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili

kulikuwa kwa kiwango kizuri kwani watahiniwa 677,495 ambao ni sawa na asilimia 72.23 waliweza kuchagua jibu sahihi *A, uingizaji na usafirishaji bidhaa nje ya nchi*. Watahiniwa hawa walikuwa na uelewa kuwa ili biashara iwe ya kimataifa ni lazima kuwe na ununuzi wa bidhaa kutoka nje ya nchi na uuzaji wa bidhaa kwenda nje ya nchi.

Aidha, kipotoshi *C, usafirishaji bidhaa kwenda nje ya nchi tu*, kilivutia watahiniwa 83,179 (8.87%) na kipotoshi *B, uingizaji bidhaa toka nje ya nchi tu,* kilivutia watahiniwa 62,300 (6.64%). Watahiniwa waliochagua kipotoshi 'B' na 'C' walishindwa kuelewa kuwa biashara ya kimataifa inahusisha nyanja mbili yaani uingizaji na usafirishaji bidhaa nje ya nchi na si uingizaji bidhaa toka nje ya nchi tu au usafirishaji bidhaa kwenda nje ya nchi tu.

Vilevile, watahiniwa 65,304 sawa na asilimia 6.96 walichagua kipotoshi *D, kufanya biashara kwa kutumia pesa* na watahiniwa 43,247 sawa na asilimia 4.61 walichagua kipotoshi *E, kukopa fedha kutoka nje ya nchi* hali inayoonyesha kuwa hawakuelewa matakwa ya swali kwani vipotoshi hivyo havihusiani na maana ya biashara ya kimataifa. Hata hivyo, watahiniwa 6,470 sawa na asilimia 0.69 hawakujibu swali hili au walichagua jibu zaidi ya moja. Kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa kimeoneshwa katika Chati Na. 21.





**Chati Na. 21:** *Inaonesha kiwango kizuri cha kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kwani asilima 72.23 walichagua jibu sahihi.*

**Swali la 40:** Ni mikoa ipi inahusika na usafirishaji kupitia bahari ya Hindi?

A Mwanza, Pemba, Zanzibar na Mtwara
B Tanga, Mtwara, Kigoma na Pwani
C Zanzibar, Pemba, Mwanza na Kigoma
D Kilimanjaro, Kigoma, Tanga na Zanzibar
E Dar es Salaam, Tanga, Mtwara na Zanzibar

Swali hili lilitoka katika mada ya *Mawasiliano, Biashara na Uchukuzi.* Watahiniwa walitakiwa kubainisha mikoa inayohusika na usafirishaji kupitia bahari ya Hindi. Kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kulikuwa kwa kiwango cha wastani kwani watahiniwa 557,389 ambao ni sawa na asilimia 59.42 waliweza kuchagua jibu sahihi *E, Dar es Salaam, Tanga, Mtwara na Zanzibar*. Watahiniwa waliochagua jibu sahihi walikuwa na uelewa wa kutosha juu ya mikoa inayopakana na bahari ya Hindi ambayo ina bandari hivyo kuwezesha usafirishaji kupitia bahari husika.

Watahiniwa wengine walichagua vipotoshi kama ifuatavyo: kipotoshi *A, Mwanza, Pemba, Zanzibar na Mtwara,* kilivutia watahiniwa 102,556 (10.93%); kipotoshi *B, Tanga, Mtwara, Kigoma na Pwani*, kilivutia watahiniwa 100,984 (10.77%); kipotoshi *C, Zanzibar, Pemba, Mwanza na Kigoma* kilivutia watahiniwa 102,220 (10.90%) *na* kipotoshi *D, Kilimanjaro, Kigoma, Tanga na Zanzibar* kilivutia watahiniwa 68,250 (7.28%). Watahiniwa hao walishindwa kuelewa kuwa baadhi ya mikoa iliyopo katika orodha za chaguzi hizo haipakani na bahari ya Hindi. Kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa kimeoneshwa katika chati Na. 22.





**Chati Na. 22:** *Inaonesha kuwa kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kulikuwa kwa kiwango cha wastani kwani ni asilimia 59.42 ya watahiniwa walichagua jibu sahihi.*

## 2.2. Sehemu B

**Swali la 41:** Mfumo wa uongozi unaofuata na kuzingatia misingi ya haki na sheria huitwa ______________________

Swali hili lilitoka katika mada ya *Demokrasia* mada ndogo ya Utawala Bora. Watahiniwa walitakiwa kutaja mfumo wa uongozi unaofuata na kuzingatia misingi ya haki na sheria kwa kuandika jibu sahihi katika nafasi iliyoachwa wazi. Lengo la swali hili lilikua ni kuwapima watahiniwa uelewa kuhusu dhana ya utawala bora. Kama ilivyooneshwa kwenye Chati Na. 24, kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kulikua kwa kiwango hafifu kwani watahiniwa watahiniwa 181,706 (19.37%) tu walipata alama 2.0. na 756,089 (80.61%) walipata alama 0.0.




**Chati Na. 23** *Inaonesha kufaulu hafifu kwa watahiniwa katika swali hili kwani ni asilimia 19.37 tu ya watahiniwa waliweza kuandika jibu sahihi.*

Watahiniwa waliopata alama 0 (80.61%) walishindwa kuelewa mahitaji ya swali ambapo wengi walijibu kinyume na mahitaji ya swali Kwa kuandika demokrasia. Watahiniwa hawakufahamu kwamba demokrasia ni mfumo wa serikali ambao mamlaka yake kisiasa yapo chini ya wananchi, ni mfumo wa uongozi ambao unaruhusu watu kutoa maoni na kuamua mambo yao. Kiuhalisia, demokrasia ni nguzo mojawapo ya utawala bora. Nguzo nyingine za utawala bora ni pamoja na utawala wa sheria, kuepuka rushwa, kuheshimu haki za binadamu, ushirikishaji wa raia, uwajibikaji, uwazi na kadhalika. Pia watahiniwa wengine walipotoka kwa kuandika mifumo ya uzalishaji mali ambayo mataifa mbalimbali yamepitia kama vile Ujamaa, Ubepari, na Ukabaila. Yawezekana uwepo wa neno ‘mfumo’ kama lilivyotumika katika swali limewapa changamoto kubwa katika kulijibu swali hili.

Zaidi ya hayo, kuna baadhi ya watahiniwa waliandika majibu yasiyohitajika kabisa kama vile mfumo wa haki za binadamu, bunge, mahakama na utawala wa sheria. Watahiniwa wengine waliandika Spika wa bunge, mwanasheria mkuu wa serikali, uongozi wa serikali za mitaa na mfumo wa moja kwa moja. Kwa ufupi, watahiniwa hawa walikosa maarifa kuhusu dhana ya utawala bora, hii ndiyo sababu

iliyopelekea wajitahidi kutafuta majibu kutoka kwenye mada nyingine zinazofanana katika somo la uraia na baadhi kutoka katika somo la historia. Baadhi ya watahiniwa waliacha nafasi wazi bila kuandika majibu ya swali hili kuonesha kuwa hawakuwa na maarifa ya dhana iliyoulizwa. Kielelezo Na. 1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa yasiyoendana na matakwa ya swali.

| | |
|---|---|
| 41. Mfumo wa uongozi unaofuata na kuzingatia misingi ya haki na sheria huitwa Ni Mfumo Wa Moja Kwa Moja | |

**Kielelezo Na. 1:** *Kinaonesha jibu lisilo sahihi la mtahiniwa katika swali la 41.*


Kwa upande mwingine, watahiniwa 181,706 (19.37%) walipata alama 2.0. Watahiniwa hawa walionesha kuelewa vizuri mahitaji ya swali kwa kutaja mfumo wa uongozi unaozingatia misingi ya haki na sheria na sio aina ya serikali inayozingatia misingi ya haki na sheria. Uwezo wa hawa watahiniwa kubaini dhana iliyoulizwa katika swali ni kiashiria kwamba walikuwa na maarifa ya kutosha ya mada husika. Kielelezo Na. 2 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa mwenye maarifa ya kutosha.

| | |
|---|---|
| 41. Mfumo wa uongozi unaofuata na kuzingatia misingi ya haki na sheria huitwa Utawala bora | |

**Kielelezo Na. 2:** *Sampuli ya jibu sahihi la mtahiniwa aliyejibu swali hili.*


**Swali la 42:** Ni taifa gani lililoanza kuitawala Tanganyika baada ya vita Kuu ya Kwanza ya Dunia? ____________________

Hili ni miongoni mwa maswali yaliyokuwa na ufaulu hafifu kwani watahiniwa 576,221 (61.44%) walishindwa kuandika jibu sahihi. Watahiniwa wengi waliandika *Ujerumani*. Ujerumani iliandikwa na watahiniwa kama jibu sahihi kwa sababu walishindwa kufahamu kwamba Ujerumani lilikuwa taifa la kwanza la kikoloni kutawala Tanganyika kuanzia mwaka 1891 hadi 1918 na taifa la Uingereza lilianza kutawala Tanganyika kuanzia mwaka 1919 hadi 1961. Kwa ujumla, watahiniwa walishindwa kuandika jibu sahihi kutokana na ukosefu wa maarifa juu ya uvamizi wa Bara la Afrika mnamo miaka ya 1880.




**Chati Na 25:** *Inaonesha kufaulu kwa kiwango hafifu (38.56%) kwa watahiniwa waliofanya swali*

Hata hivyo, jumla ya watahiniwa 361,676 (38.56%) waliweza kuandika jibu sahihi *Uingereza*. Watahiniwa hao walikuwa na maarifa ya kutosha katika *Uvamizi wa Bara la Afrika*. Kielelezo Na.3 kinaonesha mfano wa majibu ya mtahiniwa aliyekuwa na uelewa wa kutosha wa mada na matakwa ya swali.



42. Ni taifa gani lililoanza kuitawala Tanganyika baada ya vita Kuu ya Kwanza ya Dunia?

TAIFA LA UINGEREZA

***Kielelelzo Na. 3*** *ni mfano wa jibu la mtahiniwa aliyeweza kuandika jibu sahihi*.

**Swali la 43:** Kwa nini Otto Von Bismarck aliita viongozi wengine kuhudhuria mkutano wa Berlin mwaka 1884?

Swali liliwataka watahiniwa kueleza sababu ya Otto Von Bismark kuwaita viongozi wengine kuhudhuria mkutano wa Berlin mwaka 1884. Ufaulu katika swali hili ulikuwa wa wastani (Angalia Chati Na. 26) kwani watahiniwa 505,942 (53.94%) waliweza kuandika hoja sahihi.




**Chati Na. 26:** *Inaonesha kiwango cha wastani cha ufaulu cha watahiniwa katika swali hili.*

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa 505,942 (53.94%) waliweza kutaja majibu sahihi *ili kuligawa bara la Afrika miongoni mwa mataifa makubwa ya Ulaya.* Otto Von Bismarck alitaka kuiepusha Ujerumani na migogoro dhidi ya mataifa mengine ya Ulaya kuhusu makoloni ya Afrika. Kwa lengo hili, aliitisha mkutano mwaka 1884 mjini Berlin wa wawakilishi wa mataifa vinara katika kugombania bara la Afrika. Kiukweli, watahiniwa hao walikuwa na ufahamu wa mchakato wa kuligawa Bara la Afrika kwani ni katika mkutano huu ambapo mataifa makubwa yaliamua maeneo ya mamlaka yao katika Afrika. Kielelezo Na. 4 kinaonesha mfano wa jibu la mtahiniwa aliyeweza kuandika jibu sahihi.

| | |
|---|---|
| 43. Kwa nini Otto Von Bismarck aliita viongozi wengine kuhudhuria mkutano wa Berlin mwaka 1884?<br>KWA SABABU ALITAKA MGAWANYO WA BARA LA-AFRIKA UFANYIKE VIZURI. | |

**Kielelezo Na. 4:** *kinaonesha mfano wa jibu la mtahiniwa aliyejibu vizuri katika swali hili.*


Uchambuzi zaidi unaonesha kwamba watahiniwa 431,963 (46.06%) walipoata alama sifuri (0) ambao hawakuwa na maarifa ya kutosha ya sababu ya Otto Von Bismark kuwaita viongozi wengine kuhudhuria mkutano wa Berlin mnamo mwaka 1884. Kielelezo Na. 5 kinaonesha mfano wa mtahiniwa aliyetoa majibu yasiyo sahihi.

| | |
|---|---|
| 43. Kwa nini Otto Von Bismarck aliita viongozi wengine kuhudhuria mkutano wa Berlin mwaka 1884?<br>Ni kwasababu alitaka mkutano huo Uwena Wranaushi wa Umoja wa mataifa | |

**Kielelezo Na. 5:** *kinaonesha mfano majibu yasiyo sahihi ya sababu za Otto Von Bismarck kuitisha mkutano wa Berlin mwaka 1884.*


**Swali la 44**: Sayari ya saba katika mfumo wa jua inaitwaje? ________________________________________

Swali lilitoka katika mada ya *Mfumo wa Jua.* Swali lilimtaka mtahiniwa kutaja sayari ya saba katika mfumo wa jua. Swali lililenga kupima maarifa ya mtahiniwa katika kujua mpangilio wa sayari zinazolizunguka jua. Kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kulikuwa kwa kiwango hafifu kwani ni watahiniwa 306,437 tu sawa na asilimia 32.67 walipata alama zote mbili (02) na watahiniwa 631,457 sawa na asilimia 67.33 hawakuweza kujibu kwa usahihi kulingana na matakwa ya swali hivyo kupata alama sifuri (0).




**Chati Na. 26:** *Inaonesha kuwa kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kulikuwa kwa kiwango hafifu kwan ni asilimia 32.67 tu ya watahiniwa ndio waliandika jibu sahihi.*


Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa watahiniwa wachache walioandika jibu sahihi walikuwa na ufahamu wa mfumo wa jua na mpangilio sahihi wa sayari katika mfumo huo. Kielelezo Na. 6 kinaonesha mfano wa jibu sahihi la mtahiniwa katika swali la 44.


44. Sayari ya saba katika mfumo wa jua inaitwaje?

ZOHARI

**Kielelezo Na. 6:** *Kinaonesha mfano wa majibu sahihi ya mtahiniwa aliyepata alama zote katika swali la 44*

Aidha, watahiniwa wengi hawakuweza kukidhi matakwa ya swali kwa kuandika sayari nyingine kama vile: Zebaki, Sumbula, Satani, na Kauri. Majibu hayo hayakuwa sahihi kwani katika Mfumo wa Jua Zebaki ni sayari ya kwanza, Sumbula ni sayari ya tano, Satani ni sayari ya sita na Kauri ni sayari ya nane. Kielelezo Na: 7 kinathibitisha baadhi ya majibu yasiyo sahihi katika swali la 44.





**Kielelezo Na. 7:** *Kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyetaja sayari ya Tano badala ya Saba.*

**Swali la 45:** Kokotoa kipimio cha ramani ikiwa umbali katika ramani ni sentimita 5 na umbali halisi katika ardhi ni kilomita 1.

______________________________

Swali hili lilitoka katika mada ya *Stadi za Ramani* na lililenga kupima uwezo wa watahiniwa kubaini kanuni na kuitumia katika kukokotoa kipimio cha ramani na kuandika jibu katika nafasi iliyo wazi.

Kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili kulikuwa kwa kiwango hafifu kwani ni watahiniwa 56,353 (6.01%) tu ndio waliweza kuonesha mchakato wa ukokotoaji wa jibu sahihi kwa mujibu wa matakwa ya swali. Watahiniwa 881,443 (93.98%) hawakukokotoa vema hivyo kushindwa kupata jibu sahihi la kipimio cha ramani kama Chati Na. 27 inavyoonesha.




**Chati Na. 27:** *Inaonesha kiwango hafifu (6.01%) cha kufaulu kwa watahiniwa katika swali hili.*

Watahiniwa wachache (6.01%) waliweza kukidhi matakwa ya swali na kupata alama zote mbili (2) katika swali hili. Watahiniwa hawa waliweza kutafsiri swali hili kwamba kama kilomita 1 ni sawa na sentimita 100,000, Je, sentimita 5 za kwenye ramani huwakilisha kilomita ngapi katika ardhi halisi? Watahiniwa waliokokotoa kwa usahihi walionesha hatua zifuatazo:

*Ufafanuzi wa swali sm 5 = km 1*

*Badili Kilometa kwenda kwenye sentimita ili vipimo vifanane*

*Km 1 = sm 100,000*

*Kwa hiyo: sm 5 = sm 100,000*


*Ili kupata kipimo sahihi cha ramani, gawanya namba ndogo kila upande:*

$$\frac{sm\ 5}{sm\ 5} = \frac{sm\ 100{,}000}{sm\ 5} = 20{,}000$$

*Kwa hiyo, kipimo cha ramani ni 1:20,000*

Watahiniwa waliofuata hatua za ukokotoaji kwa usahihi walikuwa na uelewa wa kutosha katika ukokotoaji wa kipimio cha ramani. Aidha, baadhi ya watahiniwa hawakuonesha mchakato wa ukokotoaji katika karatasi ya maswali lakini waliandika kipimio sahihi cha ramani ambacho ni 1:20,000. Watahiniwa hao pia walipewa alama zote mbili.

Uchambuzi zaidi unabaini kuwa watahiniwa wengi walishindwa kuandika kanuni ya kutafuta kipimio cha ramani ambayo ni uwiano wa vipimo vilivyotumika kwenye ramani na vipimo halisi vya kwenye ardhi. Kwa mfano, baadhi ya watahiniwa hawakuonesha kwa usahihi mchakato wa ukokotoaji wa kipimo cha ramani hivyo kupata majibu yasiyo sahihi kama vile: - 1:2,000; 1:500,000; 1:5km; 1:50,000. Pia watahiniwa wengine waliandika majibu bila kukokotoa. Kielelezo Na. 8 ni mfano wa majibu ya mtahiniwa yasiyokidhi matakwa ya swali la 45.



45. Kokotoa kipimio cha ramani ikiwa umbali katika ramani ni sentimita 5 na umbali halisi katika ardhi ni kilomita 1.

5m = ml = 100 = 5000×1
5ms = 1/kilometa 1

1 : 500000

1:500000

**Kielelezo Na 8 :** *Kinaonesha majibu ya mtahiniwa yasiyokidhi matakwa ya swali.*

## 3.0 UCHAMBUZI WA KUFAULU KWA WATAHINIWA KATIKA KILA MADA

Uchambuzi wa mada zote 28 katika mtihani wa Maarifa ya Jamii unaonesha kufaulu kwa watahiniwa kwa viwango vinavyotofautiana. Kufaulu kwa watahiniwa kulikua hafifu katika mada saba, wastani katika mada 10 na mzuri katika mada 11. Watahiniwa walibainishwa kuwa na ufaulu wa kiwango hafifu kama wastani wa kufaulu ulikuwa kati ya asilimia 0-39. Kufaulu kwa kiwango hiki kumeoneshwa katika Jedwali kwa rangi nyekundu. Vilevile, watahiniwa walibainishwa kuwa wamefaulu kwa kiwango cha wastani kama wastani wa kufaulu kwao ulikuwa kati ya asilimia 40-59. Kufaulu kwa kiwango hiki kumeoneshwa katika Jedwali kwa rangi ya njano. Kwa upande mwingine, kufaulu kwa kiwango kizuri kulianzia asilimia 60-100, ambako kumeoneshwa kwa rangi ya kijani katika jedwali.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa, kufaulu kwa watahiniwa katika baadhi ya mada kumeongezeka mwaka huu 2018 ikilinganishwa na ufaulu wa mwaka 2017. Kufaulu kwa watahiniwa katika mada tatu kumeongezeka kutoka katika kufaulu hafifu hadi kufikia kufaulu kuzuri. Mada hizo ni *Uchumi Wetu* (67.20%), *Familia Yetu* (47.46%) na *Hali ya Hewa* (47.47%), pia kuna ongezeko la kufaulu kutoka kiwango cha wastani hadi kufaulu kwa kiwango kizuri katika mada za *Alama za Taifa* (22.19%), *Ulinzi na Usalama katika Shule/Taifa* (18.84%) na *Uvamizi wa Kikoloni katika Afrika kuanzia mwaka 1880* (27.35%). Kwa upande mwingine, kufaulu kwa watahiniwa katika

mada za *Utamaduni Wetu* (41.18%) na *Vitangulizi vya Ukoloni* (25.32%) kulishuka kutoka kufaulu wa kiwango kizuri hadi kufaulu kwa kiwango hafifu kama ilivyo kwa mada za *Usomaji wa Ramani* (28.19%) na *Mazingira* (13.06%) kulikoshuka kutoka kufaulu kiwango cha wastani hadi kufaulu kwa kiwango hafifu.

Kwa ujumla, ulinganifu wa kufaulu kwa watahiniwa kwa mwaka 2018 umeonesha kuongezeka ukilinganisha na ule wa 2017, ambapo mada nyingi zilizotahiniwa zimeonesha ongezeko la kufaulu kwa watahiniwa. Hata hivyo, mada chache zimeonekana kupungua katika kufaulu kwa watahiniwa. Taarifa zaidi za kufaulu kwa watahiniwa katika kila mada zilizotahiniwa mwaka huu zimeoneshwa katika majedwali na kiambatisho.

**Jedwali Na. 13: Mada zilizoonesha ongezeko la kufaulu kwa watahiniwa**

| Na. | Mada | Wastani wa ufaulu 2017 (%) | Wastani wa ufaulu 2018 (%) | Wastani wa ongezeko (%) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Alama za Taifa | 50.0 | 72.19 | 22.19 |
| 2 | Ulinzi na Usalama katika Shule/Taifa | 47.5 | 66.34 | 18.84 |
| 3 | Uchumi Wetu | 15.1 | 82.30 | 67.20 |
| 4 | Serikali za Mitaa | 34.5 | 36.08 | 1.58 |
| 5 | Ushirikiano kati ya Tanzania na Mataifa Mengine | 20.5 | 23.95 | 3.45 |
| 6 | Familia Yetu | 33.00 | 80.46 | 47.46 |
| 7 | Uvamizi wa Kikoloni katika Afrika kuanzia mwaka 1880 | 33.45 | 60.80 | 27.35 |
| 8 | Kuanzishwa kwa utawala wa | 44.80 | 45.70 | 0.90 |

| Na. | Mada | Wastani wa ufaulu 2017 (%) | Wastani wa ufaulu 2018 (%) | Wastani wa ongezeko (%) |
|---|---|---|---|---|
| | kikoloni katika Tanganyika na Zanzibar | | | |
| 9 | Hali ya Hewa | 26.72 | 74.19 | 47.47 |

**Jedwali Na 14: Mada zilizoonesha kushuka kwa kufaulu kwa watahiniwa**

| Na. | Mada | Wastani wa ufaulu 2017 (%) | Wastani wa ufaulu 2018 (%) | Wastani wa kushuka (%) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Utamaduni Wetu | 69.6 | 28.42 | 41.18 |
| 2 | Ushirikiano wa Kimataifa | 58.90 | 56.61 | 2.29 |
| 3 | Vitangulizi vya Ukoloni | 74.10 | 48.78 | 25.32 |
| 4 | Usomaji wa Ramani | 42.8 | 14.61 | 28.19 |
| 5 | Mazingira | 52.45 | 39.39 | 13.06 |

## 4.0 HITIMISHO

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika mtihani wa Maarifa ya Jamii umeonesha kuongezeka kwa kiwango cha kufaulu kwa watahiniwa kwa asilimia 10.89 (hii ina maana kwamba, mwaka 2017 ufaulu umeongezeka kutoka asilimia 62.73 hadi asilimia 73.62). Kiwango cha ufaulu kwa watahiniwa katika mada 28 kimeongezeka kutoka ufaulu hafifu hadi ufaulu mzuri katika mada tatu ambazo ni; *Utamaduni Wetu*, *Uvamizi wa Kikoloni katika Afrika Kuanzia Mwaka 1880* na *Hali ya hewa*.

Vilevile, baadhi ya mada kiwango cha kufaulu cha watahiniwa kimeongezeka kutoka kiwango cha wastani hadi kiwango kizuri. Mada hizo ni; *Alama za Taifa*, *Ulinzi na Usalama katika Shule/Taifa*.

Zaidi ya hapo, kiwango cha kufaulu katika mada za *Utamaduni Wetu* kimeshuka kutoka kiwango kizuri hadi kiwango hafifu wakati mada ya *Vitangulizi vya Ukoloni* imeshuka kutoka kiwango kizuri hadi kiwango cha wastani. Mada ambazo kiwango cha kufaulu kimeshuka kutoka ufaulu wa wastani hadi ufaulu hafifu ni mada za *Tafsiri za Picha na Ramani, Mazingira* na *Kukua kwa Mifumo ya Kiuchumi na Kiutawala katika jamii za Kitanzania hadi karne ya 19*.

Kwa ujumla, mada za *Serikali za Mitaa* na *Mashirikiano baina ya Tanzania na Mataifa mengine* zimeendelea kuwa na kiwango hafifu cha kufaulu.

## 5.0 MAPENDEKEZO

Ili kuboresha kiwango cha elimu, hususan kufaulu kwa watahiniwa, Baraza la Mitihani la Tanzania linapendekeza mambo yafuatayo:

(a) Walimu wanaofundisha masomo ya Uraia, Historia na Jiografia yanayounda mtihani wa Maarifa ya Jamii katika shule za Msingi wanatakiwa kufundisha mada zote kwa ukamilifu kama zinavyooneshwa kwenye muhtasari.

(b) Walimu na watahiniwa wabaini mada zilizokuwa na ufaulu wa chini katika mtihani wa mwaka huu na kuziongezea bidii ikiwemo kutumia zana bora za kufundishia na kujifunzia ili ziweze kuwa na kiwango kizuri cha kufaulu katika mitihani ya miaka ijayo. Mada hizo ni; *Tafsiri za Picha na Ramani, Mazingira na Kukua kwa Mifumo ya Kiuchumi na Kiutawala katika jamii za Kitanzania hadi karne ya 19*.

(c) Watahiniwa washauriwe na kusisitiziwa kusoma kwa kina vitabu vya kiada na ziada ili kuongeza maarifa na ujuzi ambao utawawezesha kujibu maswali ya mtihani kwa usahihi.

(d) Walimu na watahiniwa wapitie taarifa ya uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika mtihani wa kumaliza elimu ya msingi inayotolewa na Baraza la Mitihani la Tanzania ili kutambua makosa ya kimazoea yanayosababisha kushindwa kufanya vizuri mitihani ya mwisho.

(e) Mamlaka husika ziendelee kufanya ufuatiliaji katika ufundishaji na ujifunzaji wa masomo ya Uraia, Historia na Jiografia, hasa wakitilia mkazo zaidi mada ambazo ufaulu wa watahiniwa umeshuka ili kubaini changamoto zinazozuia ufanisi katika ujifunzaji na ufundishaji na kuziondoa ili kuongeza kiwango cha kufaulu.

## KIAMBATISHO

### Ulinganifu wa kufaulu kwa watahiniwa katika kila mada kwa mwaka 2017 na 2018

| Na | Mada | Mtihani wa 2017 | | | | Mtihani wa 2018 | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kufaulu kwa kila Swali | | | | Kufaulu kwa kila Swali | | | |
| | | Namba ya swali | (%) ya Kufaulu | (%) Wastani wa Kufaulu | Maoni | Namba ya swali | (%) ya Kufaulu | (%) Wastani wa Kufaulu | Maoni |
| 1. | Uongozi katika Ngazi ya Familia/Shule | - | - | - | - | 1 | 68.39 | 68.39 | Vizuri |
| 2. | Uongozi wa Serikali za Mitaa | 1<br>3 | 63.80<br>21.10 | 44.70 | Wastani | 2<br>3 | 20.23<br>51.92 | 36.08 | Hafifu |
| 3. | *Serikali Kuu | 2 | 47.90 | 47.90 | Wastani | - | - | - | - |
| 4. | *Demokrasia | 9<br>10 | 56.60<br>64.30 | 60.50 | Vizuri | - | - | - | - |
| 5. | Alama za Taifa | 4<br>5 | 85.20<br>14.90 | 50.00 | Vizuri | 4 | 72.19 | 72.19 | Vizuri |
| 6. | Ulinzi na Usalama katika Shule/Taifa | 6<br>7 | 24.20<br>70.80 | 47.50 | Wastani | 11 | 66.34 | 66.34 | Vizuri |
| 7. | Uchumi Wetu | 12 | 15.10 | 15.10 | Hafifu | 5 | 82.30 | 82.30 | Vizuri |
| 8. | Utamaduni Wetu | 11 | 69.60 | 69.60 | Vizuri | 7 | 28.42 | 28.42 | Hafifu |
| 9. | Ushirikiano kati ya Tanzania na Mataifa Mengine | 14 | 20.50 | 20.50 | Hafifu | 9 | 23.95 | 23.95 | Hafifu |
| 10. | *Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. | 13 | 43.50 | 43.50 | Wastani | - | - | - | - |
| 11. | Misingi ya Demokrasia | 8 | 54.80 | 54.80 | Wastani | 6<br>8<br>10<br>41 | 61.84<br>25.53<br>81.72<br>19.37 | 47.12 | Wastani |
| 12. | Ushirikiano wa Tanzania na Tamaduni Nyingine | - | - | - | - | 12 | 49.46 | 49.46 | Wastani |
| 13. | Familia Yetu | 15 | 33.00 | 33.00 | Hafifu | 13 | 87.90 | 80.46 | vizuri |

| Na | Mada | Mtihani wa 2017 | | | | Mtihani wa 2018 | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kufaulu kwa kila Swali | | (%) Wastani wa Kufaulu | Maoni | Kufaulu kwa kila Swali | | (%) Wastani wa Kufaulu | Maoni |
| | | Namba ya swali | (%) ya Kufaulu | | | Namba ya swali | (%) ya Kufaulu | | |
| | | | | | | 22<br>23 | 80.57<br>72.91 | | |
| 14. | Chimbuko na Mabadiliko ya Binadamu | - | - | - | - | 19 | 59.61 | 59.61 | Wastani |
| 15. | Hatua za Maendeleo ya Binadamu Katika Zama Mbalimbali | - | - | - | - | 20 | 53.90 | 53.90 | Wastani |
| 16. | Kukua kwa Mifumo ya Kiuchumi na Kiutawala Katika Jamii za Kitanzania hadi Karne ya 19. | 16<br>17 | 31.50<br>52.20 | 43.35 | Wastani | 21 | 19.59 | 19.59 | Hafifu |
| 17. | Utamaduni | 19<br>20 | 35.30<br>37.20 | 36.25 | Hafifu | - | - | - | - |
| 18. | Uhusiano wa Jamii za Kitanzania na Jamii Nyingine za Kiasia na Kizungu | 22 | 31.90 | 31.90 | Hafifu | - | - | - | - |
| 19. | Biashara ya Watumwa | 18<br>23 | 23.80<br>32.60 | 28.20 | Hafifu | - | - | - | - |
| 20. | Upinzani Dhidi ya Uvamizi wa Kikoloni Tanganyika na Zanzibar | - | - | - | - | 24 | 44.35 | 44.35 | Wastani |
| 21. | Kuanzishwa kwa Utawala wa Kikoloni katika Tanganyika na Zanzibar | 31 | 44.80 | 44.80 | Wastani | 14<br>18<br>42 | 56.70<br>41.80<br>38.36 | 45.60 | Wastani |
| 22. | Vitangulizi vya Ukoloni | 24 | 74.10 | 74.10 | Vizuri | 17 | 48.78 | 48.78 | Wastani |
| 23. | Uvamizi wa Kikoloni katika | 25 | 47.50 | 33.45 | Wastani | 15<br>16 | 65.37<br>63.08 | 60.93 | Vizuri |

| Na | Mada | Mtihani wa 2017 | | | | Mtihani wa 2018 | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kufaulu kwa kila Swali | | (%) Wastani wa Kufaulu | Maoni | Kufaulu kwa kila Swali | | (%) Wastani wa Kufaulu | Maoni |
| | | Namba ya swali | (%) ya Kufaulu | | | Namba ya swali | (%) ya Kufaulu | | |
| | Afrika Kuanzia Mwaka 1880 | 27 | 19.40 | | | 43 | 53.94 | | |
| 24. | Harakati za Kupigania Uhuru katika Afrika | 26 | 21.90 | 21.90 | Hafifu | - | - | - | - |
| 25. | Mabadiliko ya Kijamii, Kisiasa na Kiuchumi Katika Afrika Huru | 28<br>29<br>30<br>32 | 59.30<br>49.90<br>42.60<br>25.50 | 44.32 | Wastani | - | - | - | - |
| 26. | Ushirikiano wa Kimataifa | 21 | 58.90 | 58.90 | Wastani | 25<br>26 | 52.00<br>61.30 | 56.61 | Wastani |
| 27. | Mawasiliano, biashara na uchukuzi | 45<br>50 | 83.3<br>60.4 | 71.85 | Vizuri | 38<br>39<br>40 | 64.52<br>72.23<br>59.42 | 65.39 | Vizuri |
| 28. | Mazingira | 33<br>37 | 84.7<br>20.2 | 52.45 | Wastani | 31<br>33<br>34 | 74.34<br>23.26<br>20.58 | 39.39 | Hafifu |
| 29. | Shughuli za Kiuchumi | 40<br>46<br>47<br>48<br>49 | 41.6<br>50.6<br>54.1<br>41.5<br>70.0 | 51.56 | Wastani | 37 | 45.85 | 45.85 | Wastani |
| 30. | Majanga | 44 | 68.5 | 68.5 | Vizuri | 27<br>28 | 53.81<br>67.29 | 60.55 | Vizuri |
| 31. | Usomaji wa ramani | 34<br>38<br>39 | 51.1<br>50.3<br>27.1 | 42.8 | Wastani | 32<br>45 | 23.22<br>6.01 | 14.61 | Hafifu |
| 32. | Maji | 36 | 65.5 | 65.5 | Vizuri | 29 | 60.84 | 60.84 | Vizuri |
| 33. | Mfumo wa Jua | 35 | 20.0 | 20.0 | Hafifu | 44 | 32.67 | 32.67 | Hafifu |
| 34. | Hali ya hewa | 41 | 17.8 | 17.8 | Hafifu | 35 | 74.19 | 74.19 | Vizuri |
| 35. | Kutegemeana katika mazingira | - | - | - | - | 30 | 71.30 | 71.30 | Vizuri |
| 36. | Idadi ya Watu na Makazi | - | - | - | - | 36 | 59.67 | 59.67 | Wastani |
| 37. | Tafsiri za Picha na Ramani. | 42 | 72.8 | 67.6 | Vizuri | - | - | - | - |